KISWAHILI

6

SANIFU KWA SHULE ZA SEKONDARI

KITABU CHA MWALIMU
KIDATO CHA SITA

TAN PRINTS

YALIYOMO

YALIYOMO	III
UTANGULIZI	IV
MPANGILIO WA MASOMO YA KISWAHILI: DARASA LA SITA MUHULA WA KWANZA	1
FUNZO: FASIHI (UK. 4)	10
FUNZO: HADITHI (UK. 4)	11
FUNZO: HADITHI FUPI: MAMA WA KAMBO (UK. 9)	12
FUNZO: RIWAYA (UK 12)	16
UCHAMBUZI WA JUMLA WA “ADILI NA NDUGUZE”	24
FUNZO: TAMTHILIA (UK 28)	35
FUNZO: TAMTHILIA:” HAWALA YA FEDHA”	36
FUNZO: USHAIRI (UK. 40)	46
FUNZO: UCHAMBUZI WA SHAIRI	47
FUNZO: TENZI (UK. 47)	52
FUNZO: NGONJERA UK - 49	53
FUNZO: ZUHALI (UK. 52)	54
FUNZO: MAJIGAMBO (UK. 53)	55
FUNZO: MNYAMBULIKO WA VITENZI (UK. 56)	56
FUNZO: UAMBISHAJI WA VITENZI (UK 73)	63
FUNZO: UTUNGAJI WA RISALA (UK. 100)	71
FUNZO: HOTUBA (UK. 101)	73
MAREJEO	76

UTANGULIZI

Mwalimu ndiye anayeweza kulifanya funzo lake kupendeza au kuchukiwa yategemea matayarisho yake na kujiendeleza kwake Katika lugha hii. Kitabu hiki kina madhumuni ya kusaidia mwalimu kutayarisha na kufundisha vizuri somo lake. Kinaweza kutumiwa pamoja na kitabu cha mwanafunzi : darasa la sita. Mwalimu anapaswa kuongeza mbinu nyingine za kuvutia somo lake kutokana na tajriba ya wanafunzi.

Wanafunzi wa darasa la sita ni wanafunzi ambao wana ujuzi mkubwa Katika lugha ya Kiswahili. Wajibu wa mwalimu ni kuendeleza na kukuza zaidi ujuzi waliwo nao kulingana na maendeleo ya kisasa. Ndiyo maana anaombwa kurejelea vitabu vingine vya kumsaidia kuboresha ujuzi wake.

Kitabu hiki kina madhumuni ya kumsaidia mwalimu kufundisha mada mbalimbali zinazotarajiwa kufundishwa Katika darasa la sita. Kwa kila mada kitabu hiki kinaonyesha shabaha, na hatua za kufuatwa wakati wa kufundisha somo la Kiswahili, pamoja na vifaa vitakavyotumiwa wakati huu. Kinatoa majibu kwa maswali yaliyoulizwa Katika kitabu cha mwanafunzi.

Kitabu hiki kina mpangilio wa somo la Kiswahili kutoka muhula wa kwanza hadi muhula wa tatu lakini unaweza kubadilika kulingana na mahitaji na namna mwalimu anavyotaka kufundisha somo lake.

Wandishi wa kitabu hiki ni Bwana Emmanuel NIYIRORA na Bwana Ladislas NDAYAMBAJE wote kutoka chuo kikuu cha Ualimu cha Kigali.

Tunawatakia heri na fanaka walimu watakaotumia kitabu hiki.

NIYIRORA Emmauel

NDAYAMBAJE Ladislas

Julai, 2012

MPANGILIO WA MASOMO YA KISWAHILI: DARASA LA SITA MUHULA WA KWANZA

WIKI	KIPINDI	FUNZO	SHABAHA	VIFAA	ukurasa	MAZOEZI YA ZIADA	UKURASA
1	1 2 3 4 5 6 7	Fasihi	-Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya fasihi. -Kuwaongoza wanafunzi kuzijua na kuzifafanua tanzu za fasihi simulizi na za fasihi andishi	Ubao Chaki kitabu	4	Kutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi	4
2	1 2 3 4 5 5 7	Hadithi	-Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya hadithi -Kuwaongoza wanafunzi kuchambua hadithi kwa kuzingatia fani na maudhui.	Kitabu Chaki ubao	5	Kuchambua hadithi	5
3	1 2 3 4 5 6 7	Hadithi	-Kuwaongoza wanafunzi kusoma hadithi fupi : Mama wa Kambo. -Kuwaongoza wanafunzi kuchambua hadithi fupi “Mama wa Kambo”	Kitabu Chaki Ubao	9	Kuchambua hadithi fupi: Mama wa Kambo	9

4	1 2 3 4 5 6 7	Riwaya	-Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya riwaya, aina za riwaya -Kuwaongoza wanafunzi kuchambua riwaya kwa kuzingatia fani na maudhui.	Kitabu Chaki ubao	12	Kujua maana ya riwaya pamoja na kuonyesha vipengele ambavyo hutumiwa katika uchambuzi wa Riwaya	27
5	1 2 3 4 5 6 7	Riwaya	Kuwaongoza wanafunzi kusoma riwaya ya Adili na nduguze	Kitabu Chaki ubao	15	Kusoma riwaya katika kitabu cha riwaya ya Adili na nduguze	1- 64
6	1 2 3 4 5 6 7	Riwaya	Kuwaongoza wanafunzi kuchambua riwaya "Adili na nduguze" kwa kuzingatia fani na maudhui	Kitabu Chaki ubao	15	Kuchambua riwaya "Adili na nduguze"	15
7	1 2 3 4 5 6 7	Tamthilia	-Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya tamthilia na aina za tamthilia - Kuwaongoza wanafunzi kuchambua tamthilia	Kitabu Chaki ubao	28	Mazoezi kuhusu tamthilia	40

8	1 2 3 4 5 6 7	Tamthilia	- kuwaongoza wanafunzi kuchambua tamthilia" Hawala ya fedha" kwa kuzingatia fani na maudhui	Kitabu Chaki ubao	33	Uchambuzi wa tamthilia "Hawala ya fedha"	33
9	1 2 3 4 5 6 7	Ushairi	-Kuwaongoza wanafunzi kujua maana na aina za ushairi	Kitabu Chaki Ubao	40	Kufanya mazoezi yanayohusiana na ushairi	52
10	1 2 3 4 5 6 7	Ushairi	Kuwaongoza wanafunzi Kuchambua aina mbalimbali za ushairi wakizingatia fani na maudhui	Kitabu Chaki Ubao	42	Kuchambua shairi	52
11 12 MITIHANI YA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA							

MUHULA WA PILI

WIKI	KIPINDI	FUNZO	SHABAHA	VIFAA	ukurasa	MAZOEZI YA ZIADA	UKURASA
1	1 2 3 4 5 6 7	Mnyambuliko wa vitenzi : Dhana na aina za vitenzi	Kuwaongoza wanafunzi kutaja dhana na aina mbalimbali za vitenzi	Kitabu Chaki ubao	56	Mazoezi kuhusu dhana na aina za vitenzi	66
2	1 2 3 4 5 6 7	Mnyambuliko wa vitenzi: viambishi	Kuwaongoza wanafunzi kujua aina mbalimbali za viambishi	Kitabu Chaki ubao	68	Mazoezi kuhusu viambishi	73
3	1 2 3 4 5 6 7	Mnyambuliko wa vitenzi: viambishi	Kuwaongoza wanafunzi kujua matumizi ya viambishi	Chaki Ubao kitabu	71	Mazoezi kuhusu viambishi	73
4	1 2 3 4 5 6 7	Mnyambuliko wa vitenzi	Kuwaongoza wanafunzi kujua matumizi ya viambishi katika vitenzi	Chaki Ubao kitabu	71	Mazoezi kuhusu mnyambuliko	88

5	1 2 3 4 5 6 7	Mnyambuliko wa vitenzi	Kuwaongoza wanafunzi kujua matumizi ya viambishi katika vitenzi	Chaki Ubao kitabu	71	Mazoezi kuhusu mnyambuliko	88
6	1 2 3 4 5 6 7	Uambishaji wa vitenzi	Kuwaongoza wanafunzi kujua na kutumia viambishi vya unyambulishaji katika vitenzi	Kitabu Chaki ubao	73	Mazoezi kuhusu mnyambuliko	88
7	1 2 3 4 5 6 7	Uambishaji wa vitenzi	Kuwaongoza wanafunzi kujua na kutumia viambishi vya unyambulishaji katika vitenzi	Kitabu Chaki ubao	73	Mazoezi kuhusu mnyambuliko	88
8	1 2 3 4 5 6 7	Uambishaji wa vitenzi	Kuwaongoza wanafunzi kujua na kutumia viambishi vya unyambulishaji katika vitenzi	Kitabu Chaki ubao	73	Mazoezi kuhusu mnyambuliko	88

9	1 2 3 4 5 6 7	Uambishaji wa vitenzi	Kuwaongoza wanafunzi kujua orodha ya viambishi katika Kiswahili	Kitabu Chaki ubao	83	Mazoezi kuhusu mnyambuliko	88
10	1 2 3 4 5 6 7	Uambishaji wa vitenzi	Kuwaongoza wanafunzi kujua orodha ya viambishi katika Kiswahili	Kitabu Chaki Ubao	83	Mazoezi kuhusu mnyambuliko	88
11-12 MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI							

MUHULA WA TATU

WIKI	KIPINDI	FUNZO	SHABAHA	VIFAA	**ukurasa**	MAZOEZI YA ZIADA	UKURASA
1	1 2 3 4 5 6 7	Uambishaji wa maneno ya Kiswahili	- Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya uambishaji. - kuwaongoza wanafunzi kuunda na kunyambua maneno Fulani kutoka maneno mengine	Kitabu Chaki ubao	88	Mazoezi kuhusu uambishaji wa maneno ya kiswahili	88

2	1 2 3 4 5 5 7	Uundaji wa maneno ya Kiswahili:- dhana ya udogo Dhana ya ukubwa na dhahania	Kuwaongoza wanafunzi kutoa dhana udogo, ukubwa na dhahania	Kitabu Chaki ubao	88	Mazoezi kuhusu uambishaji wa maneno ya kiswahili	88
3	1 2 3 4 5 6 7	Uundaji wa maneno ya Kiswahili	Kuwaongoza wanafunzi kufanya uambishaji wa vitenzi	Kitabu Chaki ubao	90	Mazoezi kuhusu uambishaji wa maneno ya kiswahili	88
4	1 2 3 4 5 6 7	Uundaji wa maneno ya Kiswahili	Kuwaongoza wanafunzi kufanya uambishaji wa majina toka vivumishi, uambishaji wa vitenzi toka vivumishi, n. k	Kitabu Chaki ubao	96	Mazoezi kuhusu uambishaji wa maneno ya kiswahili	88
5	1 2 3 4 5 6 7	Utungaji : risala	Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya risala na kujua mambo muhimu Katika utungaji wa risala	Kitabu chaki ubao	98	Mazoezi yanayohusiana na risala	100

6	1 2 3 4 5 6 7	Utungaji: hotuba	Kuwaongoza wanafunzi kutunga risala	Kitabu Chaki ubao	99	Mazoezi kuhusu hotuba	112
7	1 2 3 4 5 6 7	Utungaji wa hotuba	Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya hotuba, sifa za hotuba na muundo wa hotuba	Chaki Ubao kitabu	99	Mazoezi kuhusu hotuba	112
8	1 2 3 4 5 6 7	Utungaji wa hotuba	Kuwaongoza wanafunzi kujua na kutaja aina za hotuba	Chaki Ubao kitabu	102	Mazoezi kuhusu hotuba	112
9	1 2 3 4 5 6 7	Utungaji wa hotuba	Kuwaongoza wanafunzi kuelewa fundisho muhimu wakati wa kutoa hotuba, mahali na hali ya hewa	Chaki Ubao kitabu	104	Mazoezi kuhusu hotuba	112

10	1 2 3 4 5 6 7	Utungaji wa hotuba	Kuwaongoza wanafunzi kutoa mifano ya hotuba pamoja na kuisomea mbele ya hadhira	Chaki Ubao kitabu	111	Mazoezi kuhusu hotuba	112
11-12 MTIHANI WA MWISHO WA MWAKA							

FUNZO: FASIHI (UK. 4)

Shabaha:

- Kuwaongoza wanafunzi kuelewa maana ya Fasihi kwa ujumla pamoja na vipengele vyake.
- Kuwaongoza wanafunzi kuzijua na kuzifafanua tanzu za fasihi simulizi na za fasihi andishi

Hatua: Kazi ya mwalimu Kazi ya mwanafunzi

- Kuelezea wanafunzi dhana ya fasihi Kufuata maelezo ya mwalimu na kuuliza
- kuwaelezea wanafunzi tanzu za fasihi. maswali
- Kusomea wanafunzi kazi za Fasihi Kufuata mwalimu na kusoma
- Kuuliza maswali Kujibu maswali ya mwalimu

Vifaa vitakavyotumiwa: kitabu cha mwanafunzi

Chaki

Ubao

FUNZO: HADITHI (uk. 4)

- Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya hadithi
- Kuwaongoza wanafunzi kuchambua hadithi kwa kuzingatia fani na maudhui.
- Kuwaongoza wanafunzi kuelewa vipengele ambavyo hutumiwa katika uchambuzi wa hadithi

Taratibu:

Kazi ya mwalimu kazi ya mwanafunzi

Kuonyesha vipengele vya kuchambua Katika hadithi: - Kutega masikio na kuandika

- Wahusika
- lugha
- muundo

Mandhari na maudhui

Kuwauliza maswali kujibu maswali

Vifaa vitakavyotumiwa: kitabu cha mwanafunzi

Chaki

ubao

FUNZO: HADITHI FUPI: MAMA WA KAMBO (uk. 9)

Shabaha:

- Kuwaongoza wanafunzi kusoma hadithi fupi : Mama wa Kambo.
- Kuwaongoza wanafunzi kuchambua hadithi fupi "Mama wa Kambo" kwa kuzingatia fani na maudhui

Hatua: kazi ya mwalimu kazi ya mwanafunzi

- Kuwasomea wanafunzi hadithi Kutega masikio
- Kuwasomesha hadithi wanafunzi kusoma hadithi
- Kuwafafanulia wanafunzi maneno magumu kuuliza maneno magumu.
- Kuelezea wanafunzi vipengele vilivyotumiwa Kutega masikio na kuuliza maswali.
- Vifaa vitakavyotumiwa: kitabu cha mwanafunzi

  Chaki

  ubao

UCHAMBUZI WA HADITHI FUPI: MAMA WA KAMBO

1. MAUDHUI

a) Dhamira kuu

Dhamira kuu katika hadithi ya Mama wa Kambo ni:

- Kuteswa kwa mama wa Kambo: Kibaya alipata mateso yaliyotokana na Upendo, mama yake wa kambo (kuachishwa shule, kufanya kazi kama punda, kushambuliwa, kufukuzwa)

b) Dhamira ndogo

- Ushirika wa ndoa: Mnene alioa wanawake watatu
- Kuachika kwa ndoa: ndoa ya Mnene na Nyirabagenzi iliachika.
- Huduma mbaya za wazazi (malezi mabaya): mnene kwa kutokuwa mwangalifu hakufuata malezi ya Kibaya na mwishoni alimfukuza.
- Kutakia wengine misaada: Mzee Sembabazi alimtakia Kibaya msaada kwa kumtafutia kazi. Mpangaji wa nyumba naye alimsaidia Kibaya.
- Mapenzi: mapenzi yanadhihirishwa na Kibaya na Amina.
- Hudhuma za serikali ya kampuni ya bima: serikali na Kampuni ya bima ilifanya kazi zao ipasavyo (bila rushwa au kuchelewesha kazi).
- Dini: dini ni taasisi muhimu katika kukuza utu na ubinadamu. Misaada ya waamini wa Kiislamu wa Kibaya.
- Uwivu: Upendo alionea kijicho mafanikio yote ya Kibaya akaamua kumtesa na kumkera kwa fitina na wengine.
- Ujambazi: ndugu zake Kibaya yaani Kagabo na Gasunzu walishambulia Kibaya kwa ajili ya kumnyanganya mali yake na kumuondoa duniani.

- Kujuta: kujutia kosa baada ya kutofanikiwa katika maovu na kuangamizwa na miradhi uliotengenezwa.

Maadili:

1. Mwovu huangamizwa na matendoye: Upendo, Gasunzu na Kagabo walipata shida kwa sababu ya wivu na matendo mengine ya uovu.
2. Majuto ni mjukuu: Upendo alijutia na kosa lake.
3. Mwenyezi Mungu ndiye mwongozi wa matendo yetu: Upendo alipanga mara nyingi kumwangusha hata kumwondoa duniani Kibaya lakini hakufanikiwa.
4. Mtaka makaa ya migomba haoni kitu ila majivu tu.
5. Tamaa mbele mauti nyuma: Gasunzu na Kagabo walikuwa na nia ya kujitayarisha kwa kumshambulia Kibaya lakini walijipatia mauti ya kifo.
6. Rafiki humuoni katika dhiki: Sembabazi aliyemsaidia Kibaya, Amina:
   - Kujitegemea kwa kutumia ubima,
   - Bora kuzaa watoto wa kutunza na kuletewa malezi mema.
   - Mama wa Kambo si mama

FANI

Wahusika

Aina za wahusika:

- Wahusika wakuu: wahusika wakuu ni wawili: Kibaya na Upendo. Kibaya ni mhusika mkuu wa kweli na Upendo ni mhusika mpinzani wa Kibaya.
- Wahusika wasaidizi:
- Mzee Mnene, Gasunzu na Kagabo ni wahusika wasaidizi wa upendo.
- Nyirabagenzi, Sembabazi, Mpangaji wa nyumba, Amina ni wahusika wasaidizi wa kibaya.

- Askari, afisa wa kampuni ya bima, ni wahusika wajenzi waliogeuka wasaidizi kwa Kibaya.

Methali zilizotumiwa:

1. Siku njema huonekana asubuhi
2. Kuzaliwa mwanamke ni balaa.
3. Kazi ndiyo msingi wa uhai
4. Ng'ombe wa maskini hazai
5. Alichokipoteza Mwenyezi Mungu hakuna binadamu wa kukiongoza na alichoongoza Mwenyezi Mungu hakuna binadamu wa kukipoteza.

FUNZO: RIWAYA (uk 12)

Shabaha:

- Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya riwaya na aina za riwaya
- Kuwaongoza wanafunzi kuchambua riwaya kwa kuzingatia fani na maudhui
- Kuwaongoza wanafunzi kusoma na kuchambua riwaya.

Hatua :

Kazi ya mwalimu kazi ya mwanafunzi

Kuwaelezea wanafunzi dhana ya riwaya kufuata maelezo ya mwalimu

Kuwaelezea aina za riwaya kwa kutoa mifano Kufuata maelezo ya mwalimu na

Kuandika Katika madaftarini yao

Kuonyesha vipengele vya kuchambua Katika riwaya. kufuata maelezo ya mwalimu

- *wahusika(wakuu, wajenzi, wasaidizi)*
- *Lugha (methali, nahau, picha, ...)*
- *Muundo (mwanzo, upeo, mwisho)*
- *Mandhari na maudhui(dhamira kuu na dhamira ndogo)*

Vifaa vitakavyotumiwa:

- Kitabu cha mwanafunzi
- chaki
- ubao

FUNZO: RIWAYA "ADILI NA NDUGUZE" (uk 15)

Shabaha :

- Kuwaongoza wanafunzi kusoma riwaya ya Adili na nduguze
- Kuwaongoza wanafunzi kuchambua riwaya "Adili na nduguze" kwa kuzingatia fani na maudhui

Hatua :

Kazi ya mwalimu	**kazi ya mwanafunzi**
Kuwaongoza wanafunzi kusoma riwaya	Kusoma riwaya na kuielewa
Kufafanua maneno ambayo ni magumu	Kufuata maelezo
Kusoma riwaya pamoja na kuichambua	kufuata maelezo

Vifaa vitakavyotumiwa:

-Kitabu cha mwanafunzi

-Chaki

-ubao

UCHAMBUZI WA RIWAYA "ADILI NA NDUGUZE", Shaaban Robert.

SURA YA I: Mfalme Rai

Mfalme Rai alikuwa mtawala wan chi ya ughaibu. Mfalme huyo alikuwa na tabia kuu tatu, alikuwa:

- Msuluhifu,
- Mtunzaji wa wanyama (aliwajali na kuwahurumia) na
- Mtii kwa majini.

Ughaibu ilikuwa nchi ya ufugaji. Uchumi wa nchi hii ulitegemea mifugo. Mfalme Rai alikuwa mwenye bidii ya kazi mfuatilizi wa utendaji wa kazi. Nchi ya Ughaibu ikawa haina mwivu, goigoi na mwoga kwa sababu ya kiongozi wake, mfalme Rai aliamini kuwa "tendo hukidhi haja maridhawa" Rai alikuwa mpenda haki na asiyekubali rushwa.

SURA YA II: Siri inafichuka

Ikibali mshauri wa halmashauri ya Ughaibu na mshauri wa Mfalme Rai, alikuwa mcheshi wenye kuchukuana na watu sana. Ikibali alitumwa Janibu kwenda kuangalia malipo ya kodi. Malipo hayo baada ya uchunguzi hayakuwa na hitilafu bali yalikuwa na ziada. Akiwa Janibu, Ikibali alimwona Adili akawaadhibu kikatili manyani wawili. Ikibali alishindwa kuvumilia na kuficha siri hii akalazimika kumweleza Mfalme Rai ambaye alialika Adili aletwe mbele yake ajieleze na manyani wale wawili.

SURA YA III. Adili mbele ya Rai

Adili alikuwa mtu mwenye huruma. Ukatili alioufanya dhidi ya manyani alilazimishwa tu, hakuhiari yeye mwenyewe. Alikuwa na upendo, wakati wa kuadhibu wanyama ambao walikuwa zamani ndugu zake, alikuwa anasema

«Nala sumu ndugu zangu, msambe naona tamu,

Takalifu kubwa kwangu, kuadhibu yangu damu,

Sina raha ndugu zangu, neno hili kwangu gumu. »

Kugunduliwa kwa siri yake, kulimfurahisha Adili kwani naye alipenda ijulikane. Adili alimwelezea Mfalme Rai kisa kilichomfanya manyani wake kuadhibiwa vile.

SURA YA IV. Ndugu zake

Adili alikieleza kisa cha kuzaliwa watoto watatu; yeye mwenyewe, nduguze wawili Hasidi na Mwivu. Baba yao Faraja ambaye alipewa jina hilo kwa kuwa amewafariji wazazi wake baada ya kufiwa na ndugu yake pacha. Aliwasomesha watoto wake. Ndugu hao watatu walikuwa watu wazima «wenye vichwa vilivyofunzwa lakini mioyo yao ilisahauliwa».

Baada ya kifo cha Faraja, watoto waligawana urithi sawa. Adili aliendesha biashara vyema, akitunza hesabu zote kwani alielewa kuwa "mali bila daftari hupotea bila habari". Ndugu zake walifanya biashara nchi za nje, wakapata faida kubwa na mali yao yote ikapotea.

“Mtu kushindwa kujua pato lake mwenyewe kwaonyesha uchache wa uangalifu”.

SURA YA V. Mgawo mwingine

Kwa huruma yake Adili aliamua kugawa mali yake katika sehemu tatu. Aliwaonya ndugu zake juu ya madhara ya mtu kuendeleza ulevi na kuwa mwivu. Adili alikubali kwenda nchi za nje pamoja na ndugu zake kufanya biashara. Adili alikubali akielewa kwa dhati faida za safari kama vile hizi zifuatazo:

1. Kufajirika katika hamu,
2. Kujua namna ya kuendesha maisha,
3. Kupata elimu mpya,
4. Kuelewa tabia za watu mbalimbali,
5. Kukutana na marafiki wa kweli (mara nyingine kushinda ndugu),
6. Kupata bahati njema ugenini.

SURA YA VI. Tandu na nyoka

Adili na nduguze walitembelea miji kadhaa ya awali na walipata faida kubwa katika biashara.

Wakati wakienda miji mingine waliishiwa na maji ya kunywa baharini. Walitia nanga jabalini ili kutafuta maji. Jabalini Adili alimsaidia tandu ambaye alikuwa anashambuliwa na nyoka. Tandu aligeuka msichana alimwombea dua njema Adili imfae maishani na ahera. Alimuahidi kumsaidia naye wakati ujao apatapo matatizo.

Nyoka aliyeuawa aliwaka moto, akawa majivu na majivu yakageuka chemchemu ya maji safi. Walipata shida ya maji tena, Adili alipowaomba ndugu zake wamsindikize kutafuta maji walikataa.

SURA YA VII. Mji wa mawe

Adili alipofika mji wa mawe, alishangaa kuona watu na wanyama wote wanageuka mawe. Aliuona utajiri mkubwa alioshindwa kuuchukua. Kama alivyosema mwandishi “Fikra ya mali isiyo kadiri ni mzigo usiochukuliwa”.

Pia aliona halmashauri mbili, ya wanaume na wanawake, zote mbili zilikuwa na watu waliogeuka mawe.

SURA YA VIII. Mrithi wa mji wa mawe

Adili katika upelelezi wake alifanikiwa kuingia katika chumba kimoja ambamo alimkuta msichana aliye hai. "Msichana huyu uso wake ulikuwa umetukuka kwa uzuri uliokuwa haumithiliki". Kama uzuri ulio peponi wamajaliwa malaika karibu uzuri wote ulio duniani alijaliwa msichana huyo ……. matambo yake yalikuwa kama mfutano wa mziki.

Mshale wa mapenzi ulipenya katika moyo wa Adili na haukuacha nafasi ya mapenzi ya mwanamke mwingine.

Sifa za Mwelekevu katika shairi ni hizi zifuatazo:

1. Miguu ya msichana,

   Na mwendo aliokwenda,

   Adili alipoona,

   Moyowe ulimshinda.

2. Alikuwa na miguu,

   Mfano wa cherahani,

   Wala ulimwengu huu,

   Hajatokea kifani.

3. Alipendeza hatua

   Wakati alipokwenda,

   Chini viatu vyalia,

   Mithili kama kinanda.

4. Alikwenda kwa madaha,

   Mwanamke mwenye enzi,

   Yaliyompa furaha,

Kila mwenye kubalizi.

SURA YA IX. Mji ulivyogeuka mawe

Adili alipewa maelezo na Mwelekevu jinsi mji ulivyogeuka mawe. Mfalme Tukufu na Malkia Enzi walikuwa watawala wa nchi hii. Ufalme wao ulikuwa na utukufu na enzi. Nchi ilikuwa tajiri sana, shujaa na yenye mawaziri wenye busara. Wote waliabudu mizimu.

Mrefu, Malaika-mtume wa Mola alionya Mfalme Tukufu lazima awe mwadilifu katika matendo yake, awe mfano mzuri kwa raia wake. Alionya kuwa ibada ya mizimu matokeo yake ni maangamizi. Mfalme Tukufu hakukubali onyo la Mrefu, akaamuru Mrefu ashikwe. Mrefu kwa uwezo aliopewa na Mungu, aliizamisha miji yote ndani ya bahari na kilichokuwa na maisha chote katika fahali kiligeuka jiwe. "Walakini mapendeleo yakiachwa mbali, nuru ya fikra humulika mno siku zote juu ya kweli kuliko uongo na juu ya haki kuliko dhuluma".

Nuru hii ndiyo ilimwokoa Mwelekevu mpaka alipookolewa na Adili. Adili alichukua mali aliyoweza na maji.

SURA YA X. Kutoswa kwa Adili

Adili alipofika jahazini aliigawa mali yake kwa ndugu zake, nahodha na mabaharia. Nduguze hawakuridhika kwa sababu ya choyo chao kikubwa. Walitaka pia msichana yule wamuoe wote watatu. Adili aliwaonya kuwa «ndoa haitaki ushirika, ushirika katika ndoa ulipasa wanyama na ndege. Dunia yapaswa kuwa mahali pa kiasi siyo ulafi na uchafu. Mwanaume hakukusudiwa kuwa fahali wa kila mtamba mwanamke kuwa mtembe wa kila jogoo». Kwa chuki na wivu, nduguze walimtosa Adili baharini kama kitu kilichokuwa hakifai.

SURA YA XI. Wokovu wa Adili

Akiwa baharini Adili aliokolewa na ndege. Ndege huyu alikuwa ni tandu aliyemwokoa asiuawe na nyoka pale jabalini. Tandu alijigeuza msichana aliyeitwa Huria binti kisasi. Kisasi, Mfalme wa majini na Mjeledi, mke wake. Nyoka aliyekuwa akikimbiza tandu alikuwa Hunde, waziri wa Ngazi. Hunde alikuwa kiumbe wa mwisho katika wanaume waliokuwa na sura mbaya. Alitaka kumwoa Huria kwa nguvu.

Wanawake:

i) Mioyo yao hulemewa na haja zilizokubalika

ii) Masikio yao hutiwa uziwi kwa maombi ya haraka

iii) Na miili yao ni mawindo ya jeuri daima.

«Wanaume wana inda mbaya ufisadi unapowapofusha». Wema wa Adili ulilipwa kwa fadhili Ujijini. Alipewa kitabu cha hawala za hazina ya majini.

SURA YA XII. Nduguze kuwa manyani

Marejeo ya Adili jahazini yaliwafanya Mwivu na Hasidi waone haya. Waliangua kilio cha kusingizia ingawa «kilio cha kujisingizia hakina machozi wala matanga» kama wasemavyo Waswahili. Adili aliwatuliza nduguze akisema, «bahari haiweki amana kitu kieleacho».

Huria alitamani uovu wa nduguze Adili ulipwe kwa kifo. Adili aliwaombea msamaha alikumbuka kuwa «Damu nzito kuliko maji». Huria aliamua kuwageuza na kuwafanya manyani.

SURA YA XIII. Adhabu ya kwanza

Adili alifika salama Ughaibu ila alisahau maagizo ya Huria. Adhabu ya kwanza akaipata yeye mwenyewe. Tokea hapo aliendelea kuyaadhibu manyani yale. Huria aliamini kuwa ”adhabu kali kwa waovu, ilikuwa ndiyo ulinzi bora peke yake wa wema”. Baada ya kuyapiga manyani, Adili aliyanasihi akisema:

“Nala sumu ndugu zangu,

Msambe naona tamu,

Takalifu kubwa kwangu,

Kuadhibu yangu damu,

Sina raha ndugu zangu,

Neon hili kwangu gumu”.

SURA YA XIV. Kula na manyani

Adili aliyahadithia yale yote yaliyotokea kwa sababu naye alitaka siri yake ijulikane kwa Mfalme Rai ili aweze kuwaombea nduguze msamaha. Jitihada za kuyaokoa manyaniyale zilifanywa na Rai. Alimwandikia Huria barua ya kumtaka awasamehe akiahidi kuwa tendo

hilo lilifanya Ufalme wake kuwa rafiki ya Ufalme wa majini.

Siku hii, baadala ya kuyapiga manyani, Adili alikula pamoja nayo mezani, akayapa uhuru na kulala nayo chumbani.

SURA YA XV. Arusi

Alipoulizwa sababu yake ya kuvunja amri alipewa na Huria, Adili alimtolea barua ya Rai. Ombi la Mfalme Rai lilikubaliwa na Mfalme wa majini Kisasi. Huria aliamuru:"Tokeni katika uhawayani mrudi katika utu!" Hapo hapo Hasidi na Mwivu, nduguze Adili wakawa watu tena.

Ndugu hao wawili walishukuru sana na kahidi kuwa walikoma kutenda dhala lolote kwa ndugu yao na mtu yeyote mwingine au kitu chochote kingine kilichokuwa na maisha. Watu wote hapo walifurahi na kumwombea dua Adili azidishwe cheo.

Adili aliwavisha nduguze nguo nzuri na kwenda tena Ughaibu. Walipofika pale walikuwa na furaha kubwa sana. Waliporudi kwao Janibu njiani Adili alikutana na Mwelekevu aliyekuwa na wasichana wawili. Adili alibusiana na Mwelekevu na nduguze wakaamkiana na wasichana wenzake Mwelekevu.

Walifunga safari kuelekea Janibu. Walipofika pale Janibu walifanya arusi tatu siku moja. Adili alimwoa Mwelekevu na nduguze kila mmoja akamwoa kila mwingine mwa wasichana wale nduguze Mwelekevu. Siku hiyo ilikuwa kubwa sana kuliko zozote zingine zilizopita Janibu.

Uchambuzi wa jumla wa "ADILI NA NDUGUZE"

Utangulizi

Adili na nduguze ni riwaya iliyotungwa na SHAABAN Robert; mwandishi mashuhuri (maarufu) kutoka Tanzania. Riwaya hii ilitungwa mnamo 1952. Katika riwaya yake anashughulika na mambo mengi kuhusu tabia mbalimbali za watu. Mtunzi anatueleza kuwa tushinde uovu kwa kutenda mema yaani "Wema hauozi". Adili alimwokoa Huria wakati alipokaribia kuuwawa na Hunde. Kutokana na wema huo, Huria naye alimwokoa Adili wakati alipotoswa baharini na ndugu zake. Haya yanazingatiwa na msemo wa Kiswahili "kinifaa huangua, nitakufaa kwa mvua" au methali isemayo "Mwosha huoshwa".

1. Mandhari

Mandhari ya riwaya hii ni ya nchi ya Ughaibu, yaani nchi ya mbali. Nchi hiyo ni ya kufikirika kwa kuwa haipo katika mazingira ya kawaida. Kuna vituko vichache vilivyotokea katika nchi za kigeni zisizotajwa kwa majina na vingine vilitukia katika nchi ya majini.

2. Wahusika

Wahusika wa SHAABAN Robert katika riwaya ya Adili na Nduguze, aliwapa majina yanayowiana na tabia zao. Wale ambao hawakubadilika kitabia kama Adili, Mfalme Rai ni wahusika bapa vielezo. Wahusika Huria, Hasidi na Mwivu ambao walibadilika kitabia ni wahusika duara.

3. Wahusikana tabia zao

- Adili: shauri; onyo.
- Hasidi: mtu mwenye tabia ya kutofurahia mafanikio ya mwingine (husada)
- Mwivu: mtu menye kijicho; asiyependa mafanikio ya mwingine
- Mfalme Rai: wazo au maoni ya mtu juu ya jambo fulani

Kurai: kusema na mtu kwa maneno mazuri kwa madhumuni ya kumtaka akubali kutimiza linalotarajiwa.

- (I) kibali: ruhusa, idhini
- Mwelekevu: mtiifu; mwenye urahisi wa kukubali maelezo (mwongozo)
- Huria: mwenye uhuru wa kutenda kila jambo analotaka
- Mrefu: mwenye kimo (kipimo) kilichozidi kingine (cha kawaida)
- Mfalme Tukufu: mheshimiwa, mtu mwenye madaraka au cheo cha juu
- Malkia Enzi: utawala, utukufu
- Hunde: kiumbe cha ajabu kinachitisha
- Mfalme Kisasi: malipo kwz ajili ya tendo bayaalilofanyiwa mtu#fadhila (au fadhili).
    - Adili: ni mhusika mkuu wa riwaya hii. Alikuwa mwema, mwenye huruma, msamehevu, mvumilivu, jasiri na mfanyabiashara hodari. Tabia yake ile haikubadilika toka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Kwa hiyo, tabia yake ni mhusika bapa kielelezo.
    - Hasidi na Mwivu: ni ndugu zake Adili. Walikuwa watu wakatili, wenye tamaa, choyo kikubwa na wabadilifu kitabia, kwa hiyo ni wahusika duara.
    - Mfalme Rai: alikuwa mtawala wa nchi ya Ughaibu ambaye aliiletea nchi yake ustawi wa kiuchumi kutokana na uongozi mzuri, ufuatilizi bora wa kazi na ushauri wa kuwahimiza raia kuwa wachapakazi.
    - Ikibali: ni mshauri wa Mfalme Rain a Halmashauri yake. Alikuwa mcheshi na mtu aliyechukuana na watu kutokana na kuwatunzia haki zao.
    - Mwelekevu: ni msichana mwenye upendo wa kweli, mrembo na mwaminifu kidini na kindoa.
    - Huria: ni jini lililokuwa na uwezo mkubwa wa kutenda kila jambo lililotaka na kujigeuza sura kwa utashi wake (mhusika duara)
    - Mfalme Tukufu na Malkia Enzi: ni watawala ambao walipuuzi/walidharau ujumbe wa Mola, wakaadhibiwa kugeuzwa mawe, mji wao na raia wao.
    - Mfalme Kisasi: ni mfalme wa majini aliyewaelekeza raia wake majini kutii uongozi wa binadamu.

3. Dhamira kuu

"Mapendeleo yakiachwa mbali nuru ya fikra humulika siku zote juu ya kweli kuliko uongo, juu ya haki kuliko dhuluma na juu ya wema kuliko uovu".

4. Dhamira ndogo ndogo

a. Uongozi mzuri na ufuatilizi bora wa kazi wa Mfalme Rai uliomwezesha kuistawisha nchi ya Ughaibu katika mifugo,

b. Uchunguzi mzuri wa Ikibali uliomfanya agundue hila za Adili kuwaadhibu vikali manyani,

c. Ukalili uliochanganywa na huruma dhidi ya manyani ambao zamani walikuwa nduguze Adili,

d. Utetezi wa Adili mbele ya Mfalme Rai na kukieleza kisa cha baba yao Faraja kuwazaa ndugu watatu, Adili, Hasidi na Mwivu,

e. Mvuto wa faida za biashara safarini baada ya mgawo wa urithi wa Adili na nduguze waliofilisika,

f. Wokovu wa Tandu aliyeshambuliwa na nyoka na bahati ya Adili kupata maji safi,

g. Mji wa mawe uliokuwa na mali isiyo kadiri

h. Mapenzi ya Adili na Mwelekevu, msichana aliyekutwa hai katika mji wa mawe,

i. Habari ya mji na watu wake kugeuzwa mawekutokana na ibada ya mizimu,

j. Wivu wa nduguze Adili kumwona na mchumba na kumtosa baharini,

k. Wokovu wa Adili aliyeokotwa na Huria,

l. Marejeo ya Adili jahazini na nduguze kugeuzwa manyani,

m. Adhabu kali kwa manyani baada ya Adili kuadhibuwa mwenyewe kwa kutotii amri ya Huria.

n. Jitihada za Mfalme Rai kuokoa manyani waliokuwa nduguze Adili,

o. Ombi la Mfalme Rai lililokubaliwa na Mfalme wa majini Kisasi na bintiye Huria la kugeuza manyani kuwa watu tena na ndoa ya ndugu wote watatu.

5. MHUTASARI: Adili na Nduguze

Uongozi mzuri na ufuatilizi bora wa kazi ulimfanya Mfalme Rai kuistawisha nchi yake ya Ughaibu katika mifugo. Mshauri wake Ikibali alikuwa bingwa wa uchunguzi wa kodi za wanyama ila alielemewa na siri ya kiongozi wa Janibu, Adili kuwaadhibu vikali manyani waliokuwa kwake. Alishangaa kuona jinsi ukatili huo ulivyohitilafiana sana na tabia ya wema na huruma ya Adili akaamua siri hiyo ifichuliwe mbele ya Mfalme Rai.

Alipoletwa mbele ya Mfalme Rai, Adili alijitetea akieleza kuwa wanyama hao walikuwa zamani nduguze kwani walizaliwa na baba mmoja, Faraja. Alijulisha kuwa alilazimika kuwagawia urithi wake wakati walipofilisika ugenini na kurejea nyumbani kwao Janibu. Alisimulia jinsi ndugu wote watatu walivutwa na faida za biashara na kusafiri mpaka walipoufikia mji wa mawe, Adili alipokutana na mchumba wa kuusiwa, Mwelekevu.

Hapo hapo, Adili alieleza kuwa uovu waliomfanyia nduguze ndio uliwafanya wageuzwe kuwa manyani. Kwanza kutokana na mali aliyoleta jahazini na mwanamke huyo mrembo kutoka mji wa mawe, nduguze walimwonea wivu na kumlia njama za kumtosa baharini.

Wakati huo huo, aliokolewa na jinni, Huria binti Kisasi, ambalo aliwahi kusaidia lililoshambuliwa na nyoka, ama jinni jingine Hunde.

Adili aliporejea katika chombo akiwa na Huria, jinni hilo ndipo liliamua kuwafanya manyani ikiwa ni adhabu na kutoa amri ya kuwa watapigwa kila siku kutokana na maovu yao.

Adili aliporudi nchini mwake, Ughaibu, ndiye aliadhibiwa wa kwanza kwa kusahau kuwapiga manyani. Tokea hapo ilkuwa mazoea yake kuwapa chakula na kuwapiga vikali hadi siku, Ikibali aligundua siri hiyo.

Baada ya kisa hicho, Mfalme Rai almsihi Adili asiwapige tena manyani ila awatunze vizuri na kula nao. Alijitahidi kuwaombea msamaha kwa Mfalme wa majini Kisasi na binyiye Huria. Ombi lake lilisikilizwa na nduguze Adili waligeuzwa kutoka uhawayani na kuwa watu tena. Siku hiyo ilikuwa ya furaha, na nduguze wote watatu walifunga ndoa pamoja.

6. Mtindo

Mtindo wa riwaya hii ni mtindo wa rejea. Mwandishi huanza kuisimulia riwaya yake wakati Adili alifanya ukatili wa kuwaadhibu manyani (ambao walikuwa nduguze).

Kugundulika kwa uovu huu ndiko kulifuatiliwa na maelezo ya kisa na sababu ya nduguze kuwa manyanina hatimaye kuwa watu tena baada ya ombi la Mfalme Rai kukubaliwa na majini.

Lugha ya Shaaban Robert katika riwaya ya Adili na nduguze ni nzito. Ni lugha yenye msamiati mgumu, misemo isiyo ya kawaida, nahau na methali nyingi. Pia ametumia lugha ya ushairi, lugha ya picha na tamathali za usemi za kipekee. Kuna wakati mwandishi huyu alipotumia lugha ya kisheri katika barua, na hayo yote ni kuonyesha jinsi ana ustadiwa kuimudu lugha ya Kiswahili katika nyanja zake zote.

Matumizi ya lugha

a) Tamthali za usemi

- Tashbiha:

Uk. 1: Tabia yake ijigawa katika theluthi tatu mbalimbali kama rangi ya ngozi ya pundamiliya.

Uk. 27: Aliwapenda kama penzi ya maisha yake mwenyewe.

Uk. 33: Aliwapenda kama punzi ya maisha yake.

Alikuwa na miguu mfano wa charahani.

- Sitiari:

Tamaa kwake ni gurudumu la maisha

Lugha ni pandamizi kubwa kwa watu duniani.

Adili alitamka kuwa maisha ni safari na duniani ni matembezi.

- Kipanafsi: “Moyowe ulimshinda”

Msanii amechukua moyo kama mtu.

Moyo ulimshinda ni kusema hakuweza kuzivumilia hisia za moyo wake. Kwani bila kujitambua alinaswa na uzuri wa Mwelekevu, binti Mfalme Tukufu.

b) Matumizi ya methali na nahau

i) Methali

- Mali bila daftari hupotea bila habari,
- Wema hauozi,
- Asiyefurahia heri ya mwenzake shauri yake hunghadhabika,
- Mkulima alikuwa mmoja siku zote lakini walaji wengi,
- Damu nzito kuliko maji,
- Ng'ombe wa masikini hazai picha,
- Busara kubwa kichwani haina faida kama moyoni.

ii) Nahau

- Kukata tama: kupoteza matumaini
- Macho yao yalii.

c) Matumizi ya mashairi

1. Miguu ya msichana,
   Na mwendo aliokwenda,
   Adili alipoona,
   Moyowe ulimshinda.
2. Alikuwa na miguu,
   Mfano wa cherahani,
   Wala ulimwengu huu,
   Hajatokea kifani.

Msanii alitumia ushairi kueleza kwa usanii uzuri wa Mwelekevu.

7. Muundo

Muundo wa riwaya hii unaambatana na kisa kinachomhusu Adili na nduguze, Hasidi na

Mwivu. Mwandishi alieleza jinsi vituko vilivyotiririka tokea mwanzo, ndugu hawa watatu waliokuwa wakitoka familia moja, uovu ndugu wawili, Hasidi na Mwivu, waliomfanyia Adili na malipo ya uovu huo (kama upeo wa kugeuzwa manyani na kupata adhabu ya kupigwa kila siku). Mwishoni kabisa anaujadili msamaha waliopewa ndugu hao. Kutokana na majuto na ahadi ya kutorudia tena uovu huo.

8. Maadili

- Wema hauozi (mt),
    - Kazi ni msingi wa maendeleo (ms),
    - Tendo hukidhi haja maridhawa (ms),
    - Hulka njema sawa na mali (ms),
    - Damu nzito kuliko maji (mt),
    - Mali bila daftari hupotea bila habari (ms),
    - Mbwa wa msasi mkali ni wakali pia (mt),
    - Mapendeleo yakiachwa mbali nuru ya fikra humulika siku zote juu ya kweli kuliko uongo, juu ya haki kuliko dhuluma na juu ya wema kuliko uovu (ms),
    - Turufu huenda siku zote kwa mchezaji (mt),
    - Chama chema huvikwa pete (mt),
    - Wema utashinda na ubaya utashindwa.

9. Uhakiki

Mwandishi Shaaban Robert amefaulu kuieleza hadithi yake kwa mpangilio bora wa visa vyake akianzia kuwaletea wasomaji shauku ya kujiuliza “Manyani yanapigwa kwa sababu gani? Na yahusiaje na watu?” Amewachora vizuri wahusika wake akiwapa majina yanayowiana na tabia zao. Wale wenye tabia nzuri ni mfano mzuri katika jamii yaani wanafaa kuigwa. Na wahusika wenye tabia mbaya ni mfano wa kupigwa marufuku, usiofaa kuigwa katika jamii.

Masahihisho ya maswali

1. Riwaya ni hadithi ndefu kutosha iliyoandikwa. Huwa na mchangamano wa matukio, yaani ndani yake kuna matukio mengi. Riwaya ina dhamira zake, wahusika, muundo wake na mtindo wa aina yake.

Kwa upande mwingine, Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni, ambayo huwa inakusudia kuifikia hadhira kwa kupitia njia ya maandishi. Riwaya aghalabu huwa na maneno yanayozidi 30, 000. Riwaya ina dhamira zake, wahusika, muundo wake na mtindo wa aina yake.

2. Riwaya huhifadhiwa kwa maandishi ili isisahaulike. Riwaya kwa kawada huhifadhiwa kupitia maandishi kwa sababu ya urefu wake.

3. Sifa za wahusika kutokana na namna wanavyotumiwa katika kazi yoyote ya sanaa tunapata wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi.

- Wahusika wakuu

Wahusika hao, ambao kwa kawaida ni mmoja au wawili hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Mara kwa mara wahusika hawa hubeba kiini cha dhamira kuu na maana ya hadithi yote katika wahusika wa hadithi za tanzia, wahusika wengi huonyesha mabadiliko mengi kama vile anguko pia mhusika hufikia kilele na mwisho akaanguka. Pengine mhusika anaweza kuonekana anapanda na kuwa mashuhuri, na halafu akakuwa duni katika hadithi. Wahusika wakuu wanaweza kuwakilisha vikundi, jamii au mtu binafsi.

- Wahusika wajenzi

Pamoja na kuwepo kwa wahusika wakuu, wapo pia wahusika wajenzi. Wahusika hao ni muhimu sana kama walivyo wahusika wakuu katika kazi ya sanaa. Wakati mwingine wahusika wa aina hii hujengwa sambamba na wahusika wakuu katika juhudi ya kuwajenga na kuwafafanua vizuri zaidi wahusika wakuu. Kuweko kwa wahusika hao kunasaidia sana kuipa hadithi ama kazi nyingine ya sanaa mwelekeo muhimu wa kisanaa na maudhui. Wahusika hao wana tabia ya kujitokeza mara moja moja. Kwa jumla wahusika wote hawa wana tabia ya kuhusiana na kutegemeana. Wanasaidia kukuza, kudumaza ama kufanya maamuzi muhimu ya hadithini.

Tabia za wahusika

Kutokana na sifa za wahusika tulizowaona hapa juu, tunaweza kupata tabia za wahusika za

aina tatu. Tabia hizo ni za ubapa, uduara na ufoili.

i) Ubapa: ubapa huwakilisha aina moja tu ya tabia kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Toka mwanzo hadi mwisho tabia hii inajidhihirisha katika mhusika anayeishi katika wazo na sifa za aina moja bila kubadilishwa na wakati, mazingira, uhusiano wao na wengine, n. k. Tabia hiyo haibadiliki kufuatana na hali za kawaida za maisha ya binadamu zinazobadilika kihistoria. Tabia hii inaelezwa kwa kutumia wahusika bapa-sugu na wahusika bapa vielelezo.

Wahusika bapa-sugu ni wale ambao wanaonyesha msimamo wao kutokana na maelezo ya msanii. Wanakuwa sugu katika maana kwamba hawabadiliki, kila wanapoonekana hali zao huwa ni zile zile, hawahukumiwi bali huhukumu tu, hawashauriwi bali hushauri tu, hawaongozwi bali huongoza tu.

Wahusika bapa-vielelezo kwa upande mwingine ni wale ambao pamoja na kutobadilika kwao, wanapewa majina ambayo humfanya msomaji aielewe tabia na matendo ya mhusika huyo.

Wahusika bapa hawawakilishi hali halisi ya tabia za watu wanaoishi, kwa kawaida huonyesha kipengele kimoja tu cha tabia hata kama wanakutana na mazingira mbalimbali.

ii) Uduara: uduara ni tabia ambayo mhusika mmoja hujenga akionyesha tabia tofauti. Wahusika wa aina hii wanaonyesha aina mbalimbali za tabia katika hadithi ama kazi nyingine japokuwa nazo haziwi zote zinazomhusu binadamu. Tabia ya uduara humfanya mhusika kubadilikabadilika kihulka, kimawazo na kisaikolojia.

Wahusika wenye tabia hiyo huonyesha kubadilika ambako kunatokana na msukumo wa nguvu zilizomo katika mazingira mapya. Sifa kuu ya wahusika wenye tabia hiyo, hadithini huishi maisha kawaida yanayofanana sana na jamii kiasi ambacho msomaji huwakubali kuwa ni wahusika hai.

iii) Ufoili: ufoili ni tabia inayojidhihirisha kati ya wahusika duara na wahusika bapa. Lakini pia ni tabia inayoonyesha hali zaidi kuliko wahusika bapa. Ili waweze kujengeka vyema, wahusika wenye tabia hii huwategemea sana wahusika duara na wahusika bapa. Kwa hiyo, wahusika wenye tabia ya ufoili wana msukumo wa nafsi ulio tofauti na wahusika wakuu ama wahusika wengine muhimu katika kazi ya sanaa.

4.

a) Mandhari katika riwaya ni mahali ambapo hadithi yenyewe imetokea ikiwa ni mjini, kijijini, polini au mahali pengine panapoonekana ambapo vitendo vinaweza kutokea.

b) Upeo wa riwaya hupatikana wakati hisia za msomaji zinapovutwa na anapata mchomo kiasi cha haja yake kukidhiwa.

c) Mwisho wa riwaya ndipo msomaji hutazamia ufumbuzi wa maswala yaliyoibushwa. Kuna riwaya ambazo huwaacha wasomaji wakielea na kuwafanya wafikiri katika kutafuta suluhisho. Riwaya huweza kuchukua mitindo mbalimbali. Kwa mfano, kuna ambazo mwisho huwa mwanzo na mwanzo huwa mwisho.

Kwa upande mingine, mwisho wa riwaya ni visa vyote vinavyofuata upeo ambavyo husababisha namna riwaya inapomalizika pamoja na matokeo yake. Kama kawaida riwaya ina mwanzo na mwisho ambapo msanii anaanza kuonyesha kilichomfanya kutunga kazi ya sanaa na kumalizia kwa kuonyesha hadhira namna kisa fulani kilivyotokea na suluhisho lake. Sehemu hii inachukuliwa kama mwisho wa riwaya.

5. Lugha itumikayo katika riwaya ni aina ya nathari (maandishi ya moja kwa moja, maandishi ya kawaida) na hutumia mchanganyiko wa vipengele vya lugha kama vile tamathali za usemi, methali, nahau, mafumbo, kejeli, ishara, n. k.

6. a) Mambo ambayo hujenga Riwaya ni fani na maudhui.

- Maudhui: ni yale yaliyomo ndani ya riwaya au dhamira zote na ujumbe tunaobaki nao baada ya kuisoma. Maudhui yaani mafunzo, falsafa, n. k. yatokanayo na riwaya nzima.

Maswali ya kujiuliza:

- Je, kichwa cha riwaya kinasadifu maudhui?
- Tumeambiwa nini? Yale tunayoambiwa yana ukweli wa maisha?
- Sehemu gani imetufurahisha au kutusikitisha zaidi?
- Sehemu gani haitufai au inatufaa?
- Fani: Jinsi riwaya ilivyojengeka. Kitu muhimu katika fani ya riwaya ni uchoraji

wa wahusika. Lugha ya mjazo ndicho chombo cha kuibushia maudhui. Riwaya huwa na mtiririko wa vituko. Jinsi tukio moja linavyoathiri jingine ndivyo riwaya inavyosukumwa mbele.

b) Wahusika bapa huwakilisha aina moja tu ya tabia kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Toka mwanzo hadi mwisho tabia hii inajidhihirisha katika mhusika anayeishi katika wazo na sifa za aina moja bila kubadilishwa na wakati, mazingira, uhusiano wao na wengine, n. k. Tabia hiyo haibadiliki kufuatana na hali za kawaida za maisha ya binadamu zinazobadilika kihistoria. Tabia hii inaelezwa kwa kutumia wahusika bapa-sugu na wahusika bapa vielelezo.

FUNZO: TAMTHILIA (uk 28)

Shabaha:

- Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya tamthilia na aina za tamthilia
- Kuwaongoza wanafunzi kuchambua tamthilia
- Kuwaongoza wanafunzi kujua tofauti baina ya michezo ya fasihi simulizi na fasihi andishi

Hatua:

Kazi ya mwalimu	kazi ya mwanafunzi
Kueleza maana ya tamthilia	kufuata maelezo
Kuwaonyesha wanafunzi vipengele ambavyo hutumiwa	kufuata maelezo

katika uchambuzi wa tamthilia:

a) Fani(muundo, mtindo, wahusika, mandhari na migogoro)

b) Maudhui(dhamira kuu, dhamira ndogo)

Vifaa vitakavyotumiwa:

- Kitabu cha mwanafunzi
- ubao
- chaki

FUNZO: TAMTHILIA:” HAWALA YA FEDHA”

Shabaha:

- Kuwaongoza wanafunzi kusoma tamthilia “Hawala ya fedha”
- Kuwaongoza wanafunzi kuchambua tamthilia” Hawala ya fedha” kwa kuzingatia fani na maudhui

Hatua:

Kazi ya mwalimu kazi ya mwanafunzi

Kuwaongoza wanafunzi kusoma tamthilia Kusoma tamthilia

Kuwasaidia wanafunzi kuchambua tamthilia kufuata uchambuzi wa tamthilia

kuwaonyesha wanafunzi mbinu za uchambuzi kufuata maelezo ya mwalimu

Vifaa vitakavyotumiwa: -kitabu cha mwanafunzi

- kitabu cha tamthilia ya Hawala ya fedha
- chaki
- ubao

UCHAMBUZI WA TAMTHILIA "HAWALA YA FEDHA"

Mwandishi: Amandina Lihamba

Hawala ya fedha ni tafsiri ya kitabu cha Sembene OUSMANE kinachoitwa"Le Mandat" (The money order katika lugha ya Kiingereza).

1. Mhutasari wa tamthilia "Hawala ya fedha"

Familia ya mzee Ibrahim CHANDE imetumiwa hawala ya fedha na mpwawe Abdul.

Huyu anasomea mjini London. Thamani ya hawala hiyo ni shilingi elfu mbili. Ibrahim CHANDE anapaswa kuchukua kiasi cha shilingi mia tatu, kumpatia mama yake Abdul mia tano na zinazobaki amwekee mpwa wake.

Hawala hii inaleta matumaini katika familia ya Ibrahim CHANDE, wanafikiri kwamba umasikini na njaa vimemalizika. Kwa kuwa wake zake CHANDE wamesomesha barua inayohusu hawala ya fedha, majirani wote wanajua habari hiyo.

Watu kadha wa kadha wanakuja kukopesha fedha na chakula kwenye familia hiyo. Wengine wanafuata Ibrahim CHANDE kila anapokwenda ili awasaidie kutokana na fedha hizo.

Inambidi Ibrahim CHANDE aende kubadilisha hawala yake kwenye posta. Anapofika anaombwa kuwa na kitambulisho lakini anakikosa. Hana kitambulisho chochote kila ila kadi ya chama isiyo na picha. Lazima aende kwenye kituo cha polisi.

Anapofika, anaelezwa kuwa hawezi kuwa na kitambulisho kama hana picha. Ibrahim CHANDE anamwendea AMBROZI ambaye anampiga picha. Anamwambia kurudi kesho yake baada ya kulipa shilingi thelathini. Lakini anaporudi huyu AMBROZI anamnyanganya picha pamoja na faranga zake.

Siyo hayo tu, bali anampiga vibaya pia. MBAYE anajitolea kumsaidia CHANDE kutoa fedha kwenye posta. Kwa upande mwingine, dada yake CHANDE, yaani Mama Abdul anakuja kudai faranga zake zilizoelezwa kwenye barua iliyokuja pamoja na hawala hiyo.

Mzee huyo lazima auzishe herein za dhahabu za mkewe ili dada yake asiende mikono mitupu.

Ibrahim CHANDE hapumziki hata kidogo. Mwishowe, MBAYE aliyejidai kumsaidia anamwambia kuwa fedha alizichukua kutoka posta lakini akazinyanganywa na wizi akiwa njiani.

Matumaini yote ya Ibrahim CHANDE pamoja na wake zake yakafifia. Amne mke wake wa pili akaamua kwenda zake na Mama Dogo, mke wake wa kwanza akaenda kijijini kulima shamba.

2. Wahusika

a) Wahusika wakuu

Ibrahim CHANDE ndiye anakuwa mhusika mkuu katika tamthilia "Hawala ya fedha". Ana wake wawili: MAMA DOGO na AMNE. Habadiliki kitabia tangu mwanzo hadi mwisho wa mchezo, yeye ni mhusika bapa.

Ubapa wake unadhihirishwa na ujinga wake anaokumbana nao katika habari yote. Mhusika huyu hajui kusoma wala kuandika. Isitoshe, hataki pia wake zake wawe na kisomo (uk. 4). kama inaruhusiwa katika dini ya Islam, Ibrahim CHANDE ana wake wawili. Katika usemi wake wote kuna rejesta ya dini. Pengine anaonekana akitoa sadaka kwa maskini, wengine anakataa kuwapa.

Isipokuwa ujinga wake wa kutojua kusoma na kuandika, mzee huyu anaonyesha moyo wa kusikiliza shida za watu wengine hasa hasa wale wanaotaka msaada kutoka kwake.

b) Wahusika wasaidizi

i) Mama Dogo: Huyu ni mke wake wa kwanza wa Ibrahim CHANDE. Yeye na Amne wake wenza. Hali yao ya uke wenza haiwatenganishi wala kuwafanya wachukuiane. Wanaonyesha ushirikiano tangu mwanzo hadi mwisho wa mchezo.

Mama Dogo anaonyesha busara katika maneno yake. Mfano bayana ni usemi wake unaokuwa kwenye ukurasa 41 (uk. 41), pale ambapo anasema:"Afugaye punda lazima ampendelee mlimaji nyasi. "

Katika usemi huu alitaka kuonyesha namna ambavyo hakuna mtu pekee anayeweza kujitoshereza. Kama mtu ana duka, anategemea wale ambao wanakuja kununua vitu katika duka hilo. Kwa sababu hiyo, mtu yeyote anapaswa kutodharau mwenzake.

Kila wakati, Mama Dogo anaonekana akimtetea mumewe. Anaonekana akihangaishwa na usalama wa mumewe. Ili watu wasiendelee kumfuata Ibrahim CHANDE kwa ajili ya fedha, yeye alibuni kisingizio na kuwaambia watu kuwa mume amenyanganywa fedha hizo (uk. 36-38). "Alipopata pesa watu wakamvamia (uk. 36)". "Majangili ndugu yakamvamia. Hata senti moja si yake. Mungu na Mtume, sasa pesa zimekwenda na heshima yetu pia imekwenda. "

Pengine Mama Dogo anaonyesha imani katika Mungu. Anaamini kuwa Mwenyezi Mungu hasahau waamini wake (uk. 1). yeye ndiye anaweza kunusuru maisha ya mtu aliye hatarini (uk. 37).

ii) AMNE: Huyu ni mke wa pili wa Ibrahim CHANDE, yaani mke mwenza wa Mama Dogo. Tabia yake inaonyeshwa na ushirikiano anaokuwa nao kati yake na Mama Dogo mbele ya mume wao.

Amne ana tamaa ya kuwa na kisomo. Anamwona mumewe kama mjinga wakati wowote anapomzuia kwenda kusoma. Mwishoni mwa mchezo, anaonyesha tabia ya kutoweza kuvumilia hali ya umaskini na njaa inayojitokeza katika familia yake. Alipokata tamaa ya kupata fedha zilizokuwa kwenye hawala iliyotumwa na Abdul, yeye aliamua kumtoroka mumewe.

iii) Mbarka: Ni menye duka. Kutokana na mazingira au hali mbalimbali, yeye anabadilika kitabia. Wakati alipojua kuwa Ibrahim alikuwa na hawala ya fedha, alifurahi sana na kumkopa mchele bila wasiwasi.

Lakini alipopata habari kuwa pesa za Ibrahim zimeibiwa, alikasirika na kuanza kumdai kwa fadhaa. Mbarka anaonyesha tabia za uduara.

iv) Issa: Huyu ni rafiki Ibrahim CHANDE. Urafiki wao unatokana na kuwa Issa anataka sehemu ya fedha alizonazo Ibrahim. Yeye anaonyesha tabia y unyonyaji.

Kila alipoongozana na Ibrahim wakienda mjini, alitaka Ibrahim amlipie basi. Unyonyaji wake unaonyeshwa pia na kunyang'anya watu akitumia ujanja (uk. 16). yeye alikuwa anaganda kwenye Ibrahim kama rubu ama kupe wagandavyo kwenye ng'ombe.

v) Ambrozi: Ni mwenye studio. Yeye anaonyesha tabia ya kunyanyasa watu duni. Yeye ni mjangili: anachukua pesa za watu kwa bure na kuwadhulumu ili wasije wakamdai fedha zao. Lugha anayoitumia ni ya matusi.

Amandina Lihamba alitumia katika mchezo wake wahusika wengine wa aina mbalimbali ili kuonyesha hali halisi ya maisha. Mojawapo wa wahusika hao ni bapa vielelezo.

Majina yao yanaonyesha shughuli au tabia zao. Hao ni kama mchuuzi, polisi, karani, maskini na kadhalika. Mhusika Abdul ansimamia kundi la watu waliopata kisomo. Yeye anajua umuhimu wa kusoma, ndio sababu alienda Landani.

Vilevile anajua wazazi wanahitaji msaada kutoka kwa watoto wao wakati wakiwa na uwezo. Kwa sababu hiyo, alitumia mjomba wake pamoja na mama yake hawala ya fedha.

3. Mtindo

Mtindo ni kiwango cha lugha alichotumia mwandishi katika Hawala ya fedha.

Lugha inayotumiwa ni ya mazungumzo kwani kitabu hiki ni cha mchezo wa kuigiza, yaani tamthilia.

Vipengele vya lugha vilivyotumiwa na msanii ni tamathali za usemi, nahau, methali, misemo na rejesta. Pengine alitumia lugha ya kawaida, lugha inayoeleweka kwa wazungumzaji wengi wa lugha hiyo.

i) Tamathali za usemi

a) Sitiari: mifano,

- Umaskini bila nyumba ni kifo
- Madeni yatushika mpaka pwani
- Ndiye shetani mkubwa.

b) Tashibiha

- Kukusanyika kama sisimizi, (uk. 3)
- Asiponilipa haraka nitamganda kama rubu, (uk. 16)

ii) Methali

- Kutoa ni moyo si utajiri, (uk. 13)
- Ulimi hauna mfupa: ulimi husema yote, yaani mazuri na mabaya.
- Dawa ya moto ni moto: kwa tatizo nzito lazima kauli nzito.

iii) Nahau

- Kutia chumvi,
- Chungu nzima,
- Kukata kauli,
- Kuwa na mkono mrefu (kuwa na huruma kwa kila mtu),
- Kuwa na mkono wa birika (kinyume na kuwa na mkono mrefu),
- Kukata tama,
- Kufariki dunia/kuaga dunia.

4. Muundo

Msanii alitumia muundo wa moja kwa moja, yaani hakufanya mazungumzo yanayoweza kutatanisha msomaji. Visa na matukio muhimu vya kuzingatia katika Hawala ya fedha ni hivi vifuatavyo:

- Taarifa inayomfikia Ibrahim CHANDE yenye ujumbe wa kupelekewa hawala ya fedha na kuwa postani.
- Tumaini la kuwa hawala ya fedha ingemwokoa toka hali yake ya umaskini,
- Kupanda kwa madeni,
- Harakati za kubadilisha hawala hiyo,
- Kupanda kwa tumaini la Ibrahim,
- Matumaini ya kupata vitambulisho,

- Kupatikana kwa fedha na kuibiwa kwake (Upeo wa habari),
- Kushuka chini kwa tumaini.

Msanii amefaulu kujenga kiini kimoja kutokana na mchanganyiko wa matukio mbalimbali.

5. Mandhari

Mandhari nayozungumziwa mchezoni ni halisi. Kama tulivyoelezwa na mwandishi, habari hii inatokea katika mji mdogo pwani mwa Afrika Mashariki.

6. Maudhui

Katika uchunguzi wa maudhui ya mchezo wa Hawala ya fedha tunachambua dhamira kuu pamoja na dhamira ndogo.

i) Dhamira kuu

a) Unyonyaji na kuharibika kwa urasimu

unyonyaji ni hali ya kutegemea wengine bila ya kufanya kazi; ni hali ya kuishi kwa jasho la mwingine.

Katika tamthilia Hawala ya fedha, unyonyaji unadhihirishwa na hasa hasa na majirani wa Ibrahim CHANDE wanaotaka awasaidie kwa kila hali baada ya kupata habari kuwa ametumiwa hawala ya fedha.

Kuna wanaotaka awakopeshe mchele na wengine fedha kiasi kwamba angetimiza hoja zao angebaki mikono mitupu. Mhusika anayeonekana kuwa mnyonyaji kuliko wengine ni ISSA. Huyu anamsindikiza Ibrahim CHANDE katika harakati za kubadilisha hawala ya ili apate fedha. Kila wanapoenda, ISSA anataka Ibrahim amlipie basi.

Si hayo tu, anataka ampatie fedha za kutumia katika shughuli mbalimbali. Watu wngine wanadhihirisha unyonyaji ni msichana aliyekutana na Ibrahim CHANDE akimuomba msaada kwa mara nyingi.

Pengine ni Ambrozi, aliyemnyanganya pesa zake alipoenda kujipigisha picha. Mhusika mwingine ni MBAYE aliyefaidi hawala isiyokuwa yake.

Kwa upande mwingine kuna katika mchezo huu, hali ya kuharibika kwa urasimu. Ijulikane kuwa urasimu ni utaratibu wa kuendesha kazi za kiofisi kulingana na kanuni za kiutawala.

Katika mchezo (tamthilia) Hawala ya fedha kuharibika kwa urasimu kunatambulika kutokana na viongozi (makarani).

Hawa hawafanyi kazi yao kama ilivyo. Hawakutaka kuendesha haraka mambo ya hawala ya fedha ya Ibrahim ili yeye awapatie rushwa.

b) Ujinga

Katika kitabu cha Amandina LIHAMBA, ujinga unatokana na tabia ya Ibrahim: kutojua kusoma, kukosa vitambulisho ambavyo ni mambo muhimu ya raia.

Kwa ajili ya kutojua, ilimbidhi Ibrahim kusomesha barua yake iliyohusu Hawala ya fedha. Habari hiyo ilipaswa kuwa siri lakini ilisambaa katika kijiji kizima kutokana na kuwa barua imesomeshwa.

ii) Dhamira ndogo

- Mvutano baina ya vizazi (vijana mbele ya wazazi)

Mvutano baina ya vizazi unaelezwa na msichana mmoja aliyetukana Ibrahim baada ya kujionyesha mbele yake akitaka msaada na kunyimwa. Matusi yake yalienda pamoja na kumsingizia kuwa alitaka kumtongoza.

Mvutano unaonekana pia kutokana na tabia ya Ambrozi aliyempiga Ibrahim badala ya kumpa picha zake. Alionyesha dharau kubwa mbele yake mzee.

- Nafasi ya mwanamke katika jamii

Katika nchi nyingi za Afrika, mwanamke huonekana kama kiumbe duni. Mambo yanayokuwa vilevile katika Hawala ya fedha. Ibrahim anaonyesha dharau lakini wanawake hawa wanaonekana kuwa washauri wa nafasi ya kwanza wa mume wao.

AMNE anaonekana kujikomboa kutoka dharau hiyo. Katika kitabu hiki, wanawake wengine huonekana wakitaka kusitisha mambo ya rushwa.

- Nafasi ya fedha katika maisha ya kila siku

Dhamira hii inajidhihirisha katika matukio mengi ya habari hii. Kusomesha barua lazima

fedha, kutafuta vitambulisho ni fedha, picha, chakula, safari katika basi ni mambo hay ohayo. Inadhihirika kuwa watu wote wametekwa na tamaa ya fedha ili waweze kufanya shughuli zao mbalimbali.

Mfano wa watu wanaotamani fedha kuliko wengine ni ISSA. Huyu anatumia hila ili aweze kuzipata.

Masahihisho ya maswali

1. Tamthilia huandikwa kwa madhumuni ya kuigizwa mbele ya watu, yaani kuigizwa jukwaani.
2. Aina za tamthilia ni hizi zifuatazo.
   - Ramsa: ni tamthilia zenye kuchekesha kutokana na mzaha, utani, kejeli na vitendo vya ujinga au tabia mbaya zikiwa na lengo la kuikosoa jamii, watawala na tabia mbaya za watu binafsi.
   - Tanzia: ni michezo ya kuigiza ambayo visa, vituko na migogoro yake huishia kwa huzuni, masikitiko, maanguko, hasara au kifo cha mhusika mkuu na jamii yake. Lengo la tanzia ni kuonyesha kuwa hisia zinamkera (kumuumiza) binadamu.
   - Tanzia ramsa: ni tamthilia ambazo zina mchanganyiko wa vichekesho na huzuni.

Kwa kila aina, tolea mifano kutoka tamthilia za Kinyarwanda.

3. Tanzia ni tamthilia ambayo visa, vituko na migogoro yake huishia kwa huzuni, masikitiko, maanguko, hasara au kifo cha mhusika mkuu na jamii yake. Lengo la tanzia ni kuonyesha kuwa hisia zinamkera (kumuumiza) binadamu.
4. Ramsa ni tamthilia zenye kuchekesha peke yake kutokana na mzaha, utani, kejeli na vitendo vya ujinga; wakati tanzia ramsa ni tamthilia ambazo zina mchanganyiko wa vichekesho na huzuni. Kwa hiyo, tamthilia hii hujumuisha furaha na huzuni.
5. Migogoro huifanya tamthilia isonge mbele na iwavutie hadhira kwa kiasi fulani.
6. Tamthilia ni michezo ya kuigiza ambayo huwa imeandikwa kwa makusudi ya kuigizwa jukwaani, tamthilia inajumuisha sanaa za maonyesho na michezo ya kuigiza. Tamthilia huandikwa juu ya tukio fulani na kuwasilishwa kwa watazamaji kwa njia ya mazungumzo, vitendo dhahiri na uchezaji ngoma jukwaani. Riwaya kwa upande

wake ni hadithi ndefu ya kubuni, ambayo huwa imekusudiwa kuifikia hadhira kwa kupitia njia ya maandishi. Lugha itumikayo katika riwaya ni ya aina ya nathari, yaani maandishi ya moja kwa moja.

Riwaya ikiandikwa hugawika katika sura au milango na ibara wakati tamthilia ikiandikwa au ikionyeshwa hugawika katika vipande au sehemu; na kila kipande huweza kugawanywa katika maonyesho

FUNZO: USHAIRI (uk. 40)

Shabaha:

- Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya ushairi.
- Kuwaongoza wanafunzi kujua asili ya ushairi.
- kuwaongoza wanafunzi kujua umbo la ushairi.

Hatua:

Kazi ya mwalimu — kazi ya mwanafunzi

Kuongoza na kueleza — kusoma shairi fupi

Kueleza asili na maana ya ushairi

Kuonyeshaumbo la ushairi — Kufuata na kuuliza.

a)ubeti c)mishororo e)mizani

b)vina d)kituo

kufafanua aina za ushairi — kuzijua na kutueleza.

Kusaidia na kusahihisha — kuandika majibu

Vifaa vitakavyotumiwa: kitabu cha mwanafunzi

Chaki

ubao

FUNZO: UCHAMBUZI WA SHAIRI

Shabaha: Kuwaongoza wanafunzi kujua namna ya kucha mbua shairi.

Kazi ya mwalimu Kazi ya mwanafunzi.

Kuongoza na kuhimkiza Kusoma shairi na kutambua namna ya uchambuzi.

Kuchambua shairi''Semani wenye kusema. '' Kujua na kuzingatia

a) Muundo.
b) Tamathali za usemi
c) Mpangilio wa maneno.
d) Matumizi ya picha.
e) Takriri na ridhimu
f) Dhamira na maudhoui
g) Hisia za kishairi

Kupitia funzo pamoja Kuchambua mfano.

Kusaidia na kusahihisha. Kuchambua shairi vilivyotakikana.

Uchambuzi wa jumla wa Shairi "Semani Wenye Kusema"

1. Muundo wa shairi hili:

Shairi hili lina beti sita (6). Kila ubeti una mishororo minne. Kama mashairi yanavyotungwa, shairi hili lina vina vya kati na vina vya mwisho.

i) Mizani: Shairi hili lina mizani kumi na sita. Nane upande wa ukwapi na nane upande wa uketo.

Mfano:

Mu | ko | wa | pi | we | nye | ndi | mi | , ze | nye | ma | ka | li | ya | we | mbe |?

1 2 3 4 5 6 7 8 1 2 3 4 5 6 7 8

La | da | mu | ku | ta | nga | nya | na | , za | ta | fa | u | ti | vi | u | mbe |

1 2 3 4 5 6 7 8 1 2 3 4 5 6 7 8

ii) Vina: kuna sauti (silabi) za mstari za kati na za mwisho ambazo zinafanana. Silabi hizo ndizo huitwa vina. Kuna vina vya kati na vina vya mwisho.

Mfano:

Uwovu kiwa kwa watu, ijapokuwa u tembe

Utaona kila mtu, yu mbiyoni akaimbe

Mbona leo u kwetu, twaambizana tusambe?

Msijifanye migombe, semani wenye kusema.

iii) Kituo: mstari wa mwisho wa ubeti ambao ni tofauti na mistari inayotangulia na unaomalizia beti zote za shairi ndio huitwa kituo. Kama ni ule ule unaomalizia beti zote, ni kituo kibwagizo. Katika shairi hili ni kituo kibwagizo (bahari) kilichotumiwa mwishoni mwa kila beti.

Mfano: "Msijifanye migombe, semani wenye kusema".

2. Tamathali za usemi

Katika shairi hili msanii alitumia tamathali za usemi mbalimbali kama tashbiha, sitiari, tashihisi, takriri.

a) Mshairi alitumia sitiari katika mshororo ambamo anasema:

- Muko wapi wenye ndimi, zenye makali ya wembe?
- Na wale waliyo simba, leo wangurume jumbe
- Msijifanye migombe, semani wenye kusema.

b) Mshairi pia alitumia tashbiha katikabeti zifuatazo:

Beti la kwanza

- Mbona leo hamsemi, mu kimya kama mapumbe

Beti la pili

- Hayo yaliwowafika, ni kama mefumwa chembe

c) Mshairi alitumia takriri silabi “ni”katika beti la pili, la nne, la tano na “na”katika beti la sita.

- Ni mawi yaliyotuka, ni ya ki utu msambe
- Ni yupi mwenye kutaka, kama hayo yamkumbe?
- Na kila mlima shamba, natiye mpini jembe
- Na wale waliyo simba, leo wangurume jumbe

d) Kejeli ilitumiwa sana sana katika shairi lote hasa hasa katika kituo bahari ambacho kinasema “Msijifanye migombe, semani wenye kusema”.

e) Msanii alitumia pia chuku katika shairi lake hasa hasa katika beti la sita anaposema “Lavuja paa la nyumba, wavimbaji na wavimbe Na kila mlima shamba, natiye mpini jembe Na wale waliyo simba, leo wangurume jumbe”

Katika sentensi zilizoandikwa kwa rangi iliyokoza, msanii anapiga chuku kwa kueleza fikra zake.

3. Mpangilio wa maneno

Hapa msanii alitumia lugha ya mkato, na kupanga maneno katika mpangilio wa kiima, kiarifu na shamrisho. Pia msanii alitumia mpangilio wa kuuliza maswali.

Mfano:

Ni mawi yaliyotuka, ni ya ki utu musambe

Mbona leo u kwetu, twaambizana tusambe?

Muko wapi wenye ndimi, zenye makali ya wembe?

4. Matumizi ya picha

Katika shairi hili, msanii anachora picha kwa uteuzi mzuri wa maneno ambayo yanatoa picha katika mawazo ya msemaji, anauliza maswali na kutumia maneno ambayo yanaonyesha kuwa anakasirika sana kuhusu wanavyosema. Mshairi anaonekana kuwa mwenye hasira kubwa.

Mfano:

Mwangoja yatimu kuni, halafu ndipo mulumbe

Kisikizeni kiliyo, waliyao ni viumbe.

5. Takriri na ridhimu

Kama vilivyosemwa hapo juu, msanii alitumia takriri na ridhimu kwa kusisitiza ujumbe uliotajwa.

Anatumia hasa hasa "ni" na ridhimu ambayo inaathiri mawazo na hisia za msomaji.

Katika kuchora hisi, msanii alitumia tamthali za usemi takriri na ridhimu kwa kuchora picha au taswira ya masikitiko yake katika fikra za wasomaji.

6. Maudhui na dhamira

Shairi hili linasimulia kuhusu upinzani wa msanii na watu wengine. Linaonyesha ujasiri wa msanii, imani yake na matumaini yake makubwa juu ya haki.

Msanii huyu anapigania ukweli. Shairi hili linaonyesha unyanyaswaji wa wanyonge na ukali wa msanii katika harakati za kuwakomboa.

i) Dhamira kuu

- Matumaini ya kushinda: msanii anawaita wapinzani wake waje waseme yanayomhusu. Anawahimiza kutokuwa na woga anaposema

"Muko wapi wenye ndimi zenye makali ya wembe?

Mbona leo hamsemi, mu kimya kama mapumbe?"

Dhamira kuu nyingine ambayo inaweza kuonekana hasa ni vita baina ya ukweli na uongo. Mwandishi anaonekana kuwa anataka kuonyesha ukweli wake kwa waliomsema vibaya. Kuna pia vita baina ya haki na dhuluma.

Mfano:

- Engani yatendekayo, mato yenu musifumbe

- Kisikizeni kiliyo, waliyao ni viumbe.

7. Hisia za kishairi

Hisia hizi zinaonyeshwa katika mpangilio wa maneno, picha, sauti na ridhimu pamoja na tamathali za usemi alizotumia.

Hisi inayozushwa na msanii ni kudharau watu ambao wanamsema mabaya, chuki nyingi kwa waongo.

Vifaa vitakavyotumiwa: kitabu cha mwanafunzi

Chaki

ubao

FUNZO: TENZI (uk. 47)

Shabaha: Kuwongoza mwanafunzi kujua maana, muundo na uchambuzi wa tenzi.

Kazi ya mwalimu	Kazi ya mwanafunzi
Kuongoza na kuhimiza	Kufuata mwalimu na kueleza sifa za tenzi
Kueleza maana ya tenzi	
Kutoa mifano za tenzi	Kusoma mifano na kuchambua
Kuwasaidia wanafunzi na kusahihisha	kuandika maelezo

FUNZO: NGONJERA uk - 49

Shabaha: Kuwaongoza wanafunzi kujua maana na uchambuzi wa ngonjera.

Kazi ya mwalimu Kazi ya mwanafunzi

Kuongoza na kuhimiza kutazama na kusoma kimya.

Kueleza maana ya ngongera na muundo. Kuchambua wenyewe.

Kusaidia na kusahihisha kuandika maelezo.

Vifaa: kitabu cha mwanafunzi

Chaki

Ubao

FUNZO: ZUHALI (uk. 52)

Shabaha: Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya zuhali

Kazi ya mwalimu	kazi ya mwanafunzi
Kueleza maana ya zuhali	kufuata na kuandika
Kuwagawa wanafunzi Katika makundi	kujadili kuhusu zuhali
Kusahihisha na kusaidia	kuandika maelezo

Vifaa: kitabu cha mwanafunzi

Chaki na Ubao

Majibu ya maswali

1. Utenzi au utendi ni utungo mrefu wa kishairi unaoeleza kihistoria au kisa fulani ambao hauna vina vya kati katika mistari yake, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika kila ubeti. Shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu wa lugha ya mkato katika usemi, maandishi au wimbo unaoeleza wazo au mawazo, hisi au tukio juu ya maisha na ambao hufuata utaratibu wa urari na mawala maalumu unaoheshimu na kuzingatia kanuni za ushairi unaohusika.
2. Lugha ya ushairi ni lugha inayoeleza jambo au wazo kwa njia ya mkato, kwa namna inayoteka
3. Matumizi ya vitabia katika ngonjera husaidia mhusika kufanya ishara kwa kusisitiza ujumbe.
4. Katika jamii ya Wanyarwanda hakuna utungo wa ngonjera.
5. Utungo wa utenzi huwa mrefu kwa sababu hueleza tukio muhimu la kihistoria au kisa fulani katika maisha ya binadamu. Utungo wa utenzi pia huwa na kipande kimoja.

FUNZO: MAJIGAMBO (uk. 53)

Shabaha: Kuwaongoza wanafunzi kujua muundo na washiriki Katika majigambo

Kazi ya mwalimu kazi ya mwanafunzi

Kuongoza na kuhimiza kutoa mfano wa jigambo

Kueleza muundo wa jigambo kutoa maoni yao

Kuonyesha washiriki Katika majigambo kujigamba

Vifaa vitakavyotumiwa: kitabu cha mwanafunzi

Chaki

Ubao

Fimbo

Mkuki

FUNZO: MNYAMBULIKO WA VITENZI (uk. 56)

Shabaha:

- Kuwaongoza wanafunzi kujua dhana ya kitenzi.
- Kuwaongoza wanafunzi kujua aina za vitenzi
- Kuwaongoza wanafunzi kujua viambishi awali na viambishi tamati vya kitenzi

Kazi ya mwalimu	kazi ya mwanafunzi
Kueleza dhana ya kitenzi	kutoa mifano ya vitenzi
Kuanisha vitenzi	kutambua aina za vitenzi
Kuwaongoza wanafunzi kutambua viambishi awali	kutofautisha viambishi awali

- viambishi vya kukanusha
- viambishi vya hali
- viambishi vya masharti
- viambishi vipatanishi
- viambishi rejeshi
- viambishi yambwa

Kuwaongoza wanafunzi kutambua viambishi tamati kuonyesha viambishi tamati

- Viambishi vya kauli
- Viambishi vya vimalizio
- Viambishi viulizi

Vifaa vitakavyotumiwa: kitabu cha mwanafunzi

Chaki

ubao

Majibu ya maswali

1.

a) Kitenzi kikuu: ni neno ambalo humiliki uhusiano baina ya vipashio arifu katika tungo au sentensi.

Kitenzi kikuu hubeba mambo matatu:

i) Hutoa taarifa kamili kuhusu tendo lenyewe linalofanyika,

ii) Hali ya tendo; tendo lenyewe linaweza kuwa limekamilika au linaendelea kutendeka,

iii) Kauli, yaani hapa tunapata kujua kama nomino au jina ni mtenda, mtendwa, mtendewa na kadhalika.

Kwa mfano:

- Mtoto alikuwa anacheza vizuri.
- Mwanafunzi aliwahi kusoma lakini alishindwa mitihani
- Uwase alimsindikiza hadi nyumbani.

b) Kitenzi saidizi: ni kitenzi ambacho uamilifu wake ni kukisaidia kitenzi kikuu kukamilisha uarifu wake.

Kwa mfano:

- Mtoto alikuwa anacheza vizuri.
- Mwanafunzi aliwahi kusoma lakini alishindwa mitihani
- Uwase alitaka kumuona mgeni hadi nyumbani.

2. Kitenzi ni neno linaloarifu jambo ambalo hufanywa na jina pia na kiwakilishi na kivumishi kisimamapo peke yake kama jina.

Kwa upande mwingine kitenzi ni aina ya neno linalotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu.

i) Tabia za vitenzi

Kitenzi huarifu vitu muhimu vifuatavyo:

a) Tendo lenyewe litendekalo. Kwa mfano:

- Cheza
- Anakata

b) Wakati tendo linapotendeka. Kwa mfano:

- Anakula (wakati uliopo)
- Alicheza (wakati ukliopita)
- Atafika (wakati ujao)

c) Hali ya tendo. Kwa mfano:

- Ameondoka (tendo limetimilika)
- Anasoma (tendo linaendelea)
- Kalisa huchelewa (tendo la kuzoea)

d) Masharti. Kwa mfano:

- Akija atapewa
- Ungalifika ungaliona

e) Kauli ya tendo. Kwa mfano:

- Kauli ya kutenda: Anapiga
- Kauli ya kutendwa: Anapigwa
- Kauli ya kutendewa: Anapigiwa
- Kauli ya kutendeka: Anapigika
- Kauli ya kutendana: Wanapigana

f) Kama tendo lenyewe ni la kuyakinisha au kukanusha, yaani kutenda au kutotenda. Yaani kitendo kinafanyika au haifanyiki. Kwa mfano:

- Anakula (yakinishi)
- Hakuli (kanushi)
- Unasoma (yakinishi)
- Husomi (kanushi)
- Nimefika (yakinishi)
- Sijafika(kanushi)

3. Tambulisha kitenzi kikuu na kitenzi saidizi katika sentensi zifuatazo:

Katika sentensi hizi vitenzi vikuu huandikwa kwa rangi iliyokoza wakati vitenzi saidizi huandikwa kwa mlazo.

a) Mvua kubwa imenyesha Kigali.

b) Msichana alikuwa anapika maji.

c) Kamali amewahi kufukuzwa na Nizeyimana.

d) Matofali mengi yameporomoka hapa majuzi.

e) Nunua mayai sokoni kwa haraka.

f) Mbona ulikuwa unakwenda kumtazama kaka yako usiku?

g) Pengine atakuja kuwasili leo.

h) Kitabu changu kimenunuliwa sana.

i) Anaweza kutumia anwani yetu ya posta.

j) Walikwenda kuangalia ajali ya ndege.

k) Tunaweza kukutana naye wakati wowote.

l) Mkalimani ameifasiri vizuri hotuba ya mgeni wa heshima.

m) Eti anataka kunikutana bure.

n) Faraji alikuwa anataka kumwoa Chausiku.

o) Chama cha mpira kitafanya mkutano katika Uwanja wa Taifa.

p) Pesa zangu zote zimenipotea hivi leo.

r) Huyu mvuvi amewahi kuvua nguru.

s) Murekatete ametuondoka duniani ghafla.

r) Toa hoja zako mbele ya hakimu.

4. Vishirikishi ni maneno ya aina ya vitenzi vinavyoonyesha umoja wa vitu yaani vitu kadha vipo katika hali au tabia au katika mazingira fulani.

Mifano:

- Moto unakwenda kuletwa: N+Ts+T
- Matunda yamekwenda kuchumwa: N+Ts+T
- Angalikuwa amelala: Ts+T
- Majangiri yangali yanakula nyama za karamu
- Alikuja kumchukua
- Aliweza kutambua mwenendo wake kwa urahisi.
- Angalikuwa anajifunza haungalishindwa
- Mugeni ni mwanafunzi hodari sana.
- Wawili si mmoja.
- Wafanyakazi wako ukumbini.

5. Tafuta neno linalofaa katika kila mabano ya sentensi zifuatazo na kisha lijaze katika nafasi tupu ulizopewa:

i) Wewe ndiye unayefanya kelele mtaani (ndiye, ni).

ii) Mimi siwi mwerevu kama nitawatukaneni (nawa, siwi).

iii) Kwa kweli, nyumba yangu haina ufa hata kidogo (ina, haina).

iv) Sisi tupo mbioni tu kila mara (tumo, tupo).

v) Nazi hizi zawa mbovu kwa kukaa sana (zawa, yawa).

vi) Vijana hawa hawana adabu za kutosha (hamna, hawana).

vii) Hivi ndivyo inavyotakiwa na mwalimu mkuu (ndivyo, ndicho).

viii) Kikombe kiko kabatini kama hujui (kiko, kimo).

ix) Hiki si kitabu bali ni gazeti (sicho, si).

x) Fadhili yu mkaidi wa ajabu (u, yu).

xi) Mbona siku hizi Mugabo haonekani yuko wapi? (yumo, yuko).

xii) Nyinyi mna wasiwasi wa bure (mna, wana).

xiii) Ugomvi huu ndio utakaotutenganisha mimi na mke wangu baadaye (ndio, ndiyo).

xiv) Baba yako yumo nyumbani mle (yupo, yumo).

Majibu ya maswali kuhusu viambishi

Kiambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbalimbali zinazofungamana na neno pamoja na mofimu hizo. Katika lugha ya Kiswahili viambishi huweza kujitokeza mwanzoni au mwishoni mwa mzizi.

Matumizi ya viambishi

Kwa ujumla, kama inavyoonekana viambishi vinatumika katika njia mbalimbali.

Kwanza, viambishi kama vile vya awali vinatumika katika kubadilisha umoja na wingi wa vitu tofauti.

Kwa mfano:

- Mtu – watu
- Kiti – viti
- Machungwa – chungwa
- Viatu – kiatu
- Wakulima – mkulima

Pili, viambishi awali vinatumika katika kuunganisha maneno mawili yenye maana mbalimbali kuwa na maana moja.

Kwa mfano:

- Mwana+hewa – mwanahewa
- Mchapa +kazi – mchapakazi

Tatu, viambishi awali vya majina kama vile vya ki, ji na ma hutumiwa katika mazingira kadha wa kadha.

Kwa mfano:

- Mtoto – kitoto (kuonyesha hali ya udogo).
- Mti – jiti (kuonyesha hali ya ukubwa katika umoja).
- Joka – majoka (kuonyesha hali ya ukubwa katika wingi).

Nne, viambishi awali kama vile vya ku- n a hu- katika vitenzi pia huwa na matumizi yao maalumu.

Kwa mfano:

- Kuiba kunakatazwa (kutoa maelezo).
- Hula nyama kila siku (kuonyesha mazoea).

Kuhusu viambishi tamati, baadhi ya matumizi yao yanaonekana kama ifuatavyo:

- Jirekebishe – jirekebisheni (kutoa amri).
- Ameibiwa (kuonyesha kutendwa).
- Aliniimbia (kuonyesha kutenda kwa ajili ya mtu au kitu fulani au kwa maneno mengine kuonyesha kutendewa).
- Tulikupigisha (kuonyesha dhana ya kusababisha).
- Anasemaje? (kuonyesha maulizo ya kutaka kujua kitu fulani).
- Tulikwenda dukani (konyesha mahali kwa njia ya maelezo).
- Waendapi? (kuonyesha mahali kwa njia ya maulizo).

FUNZO: UAMBISHAJI WA VITENZI (uk 73)

Shabaha: Kuwaongoza wanafunzi kuongeza viambishi mbalimbali kwenye mizizi ya vitenzi ili kuvipa maana mpya

Kazi ya mwalimu	kazi ya mwanafunzi
Kuongoza na kuhimiza	kuongeza viambishi mbalimbali
Kueleza vilivyo namna ya uambishaji	kuambisha vitenzi
	Pig
	anapigika
	Wanapigana
	Wanapiganisha

Vifaa vitakavyotumiwa:

- kitabu cha mwanafunzi
- chaki
- ubao

Majibu ya maswali

1. Viambishi awali ni- hutumika katika vitenzi kwa kuwakilisha nafsi ya kwanza umoja. Viambishi hivi huchukua nafasi ya kwanza katika kitenzi.

Viambishi tamati -ni katika Kiswahili ni viambishi ambavyo huambikwa mwishoni mwa vitenzi.

Kiambishi tamati hiki kinapoambikwa kwenye vitenzi vya Kiswahili huwa vinabeba dhana ya idadi hasa ya nafsi ya pili wingi na kutoa amri.

Mifano:

- Jirekebishe – jirekebishe-ni (kutoa amri).

- Tulikwenda duka-ni (konyesha mahali kwa njia ya maelezo).
- Ondoke-ni
- Simame-ni

Kiambishi hiki kinapoambikwa kwenye nomino, kiambishi tamati –ni hubeba dhana ya pahalaa, katika au ndani ya jina kinapoambikwa. Kama vile; mji-ni (katika mji), darasa-ni (katika/ndani ya darasa).

2. Nini maana ya "Viambishi awali", "viambishi kati" na "viambishi tamati"

   a) Viambishi awali: hivi ni viambishi vinavyosimama kabla ya kiini au shina la neno hasa kwenye majina, vivumishi, vitenzi na vielezi. Viambishi awali ni viambishi vya mwanzo. Pia, kuna viambishi vya ngeli ambavyo ni viambishi awali.

Viambishi hivi hupatikana mwanzoni mwa majina ili kuonyesha umoja au wingi wa vitu. Mifano ya viambishi awali katika aina hizo nne za maneno ni kama hii:

- mkulima mrefu ameanguka.
- mtumbwi mkubwa umezama.
- kisu kibutu kimeniumiza vibaya.
- anakula kizungu.

Viambishi awali hujitokeza pia katika mtindo wa kukanusha unaonekana katika vitenzi.

Kwa mfano :

- Sitapika
- Hukunieleza
- Hakupenda

2. Viambishi kati

Viambishi kati hupatikana mara nyingi katika vitenzi. Viambishi hivi viko namna tatu: viko viambishi wakati, viambishi rejeshi na viambishi viwakilishi vya kitendwa.

Viambishi wakati ni kama -na-, -li-, -ta-, -ka-, -ku-, -ki-, -takapo- na -ji-. Tuangalie baadhi ya mifano yao katika sentensi hizi:

- Ali anache**za mpira.**
- **Alinipiga mwizi.**
- **Tutaondoka leo.**
- **Birasa amefariki.**
- **Nikapigwa vibaya.**
- **Hawakufika ma**pema.

Viambishi wakati hujitokeza namna hii katika vitenzi:

a) Wakati uliopo

Huwakilishwa na kiambishi -na-

Mifano :

- Ninasoma : ni-na-som-a
- Sisomi : si-ɸ-som-i
- Tunalima : tu-na-lim-a
- Hatulimi : ha-tu-ɸ-lim-i

b) Wakati ujao

Wakati huu huwakilishwa na kiambishi wakati -ta-

Mifano:

- Tutasoma: tu-ta-som-a
- Nitalima: ni-ta-lim-a
- Hatutasoma: ha-tu-ta-som-a
- Sitalima : si-ta-lim-a

c) Wakati timilifu (wakati uliopita wa karibuni)

Wakati huu huwakilishwa na kiambishi -me- katika hali yakinishi na kiambishi -ja- katika hali kanushi.

Mifano:

- Nimesoma kitabu: ni-me-som-a
- Sijasoma kitabu : si-ja-som-a
- Nimekula : ni-me-ku-li-a
- Sijakula : si-ja-ku-li-a

d) Wakati uliopita (wa zamani)

Huwakilishwa na kiambishi -li- katika hali yakinishi na kiambishi -ku- katika hali kanushi.

Mifano:

- Nilisoma kitabu : ni-li-som-a
- Sikusoma kitabu : si-ku-som-a
- Tulikunywa : tu-li-ku-nyo-a
- Hatukukunywa : ha-tu-ku-ku-nyo-a

e) Wakati uliopita wa masimulizi

Mifano:

- Akaja : a-ka-ji-a
- Akaingia : a-ka-ingil-a
- Aliniuliza wakakataa : wa-ka-katal-a
- Nikamwendea, nikamuuliza, akanijibu

f) Viambishi vingine vinavyoonyesha wakati:

-nge-, -ngeli-, -ngali-, -ki-, -hu-

Mifano:

- Angekosa kazi, angeiba : a-nge-kos-a
- Asingekosa kazi, asingeiba : a-si-nge-kos-a kazi, a-si-nge-iba
- Alinikuta nikitembea : ni-ki-temb-il-a
- Walimuita akicheza : a-ki-chez-a
- Wanafunzi hupenda kunywa maji : ɸ-hu-pend-a

Viambishi rejeshi husimama baada ya viambishi vya wakati. Viambishi vyenyewe vyabadilika kadiri ya upatanisho wa kisarufi baina ya viambishi hivyo na majina ya ngeli yanayohusika.

Kwa mfano:

- Tunajiumiza.
- Anayenisumbuwa ni Mujawayezu.
- Kilichokuvutia ni hiki.

Viambishi viwakilishi vya kitendwa husimama kabla ya shina au baada ya viambishi rejeshi kama vitakuwepo.

Kwa mfano:

- Wanatusema.
- Aliyenipiga ndiye mbaya wangu.
- Tunawapenda.

3. Viambishi tamati: ni viambishi ambavyo huwekwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi au nomino.

Viko aina nyingi ya viambishi tamati. Kwa mfano:

- Twende, Twendeni.
- Mnasemaje?

- Funga, fungia, fungiana, fungwa, fungiwa, fungisha, fungika, ……

3. Tenganisha viambishi katika maumbo yafuatayo:

   - sawazisha: sawaz-ish-a
   - shikilia: shik-il-il-a
   - wasiliana: wasil-il-an-a
   - hatukumsogelea: ha-tu-ku-m-sog-il-il-a
   - hawatakukumbuka: ha-wa-ta-ku-kumb-uk-a
   - majibizano: ma-jib-il-y-an-o
   - mapenzi: ma-pend-yi
   - maombezi: ma-omb-il-yi
   - msingalijua: m-si-ngali-jua
   - mazungumzo: ma-zung-um-ur-yo
   - msahaulifu: m-sahau-l-ik-a

4. Bainisha mizizi katika maneno yafuatayo:

   - nilimwona: ni-li-mu-on-a
   - kimbiliana: kimb-il-il-a
   - mtu: m-tu
   - amehamishwa: a-me-ham-ish-w-a

FUNZO: UAMBISHAJI WA MANENO YA KISWAHILI (uk. 88)

Shabaha:

- **Kuwaongoza wanafunzi kueleza maana ya uambishaji**
- Kuunda na kunyambua maneno Fulani kutoka maneno mengine

Kazi ya mwalimu	kazi ya mwanafunzi
Kuongoza na kuhimiza	kueleza maana ya uambishaji
Kueleza dhana ya udogo na ukubwa	kutoa mifano
	Mtoto = kitoto
	Moto = jito
	Kikapu = kapu
	Mtu = jitu
Kueleza dhana ya dhahania	kutoa mifano
	Mtoto = utoto
Kuongoza kuunda maneno kutoka maneno mengine	kuunda maneno
	Kusema = usemi
	Bora = boresha
	Karibu = kukaribisha
	Zuri = vizuri

Vifaa vitakavyotumiwa:

- Kitabu cha mwanafunzi
- **Chaki**

- **Ubao**

Majibu ya maswali

1.

- Kupika = mpishi
- kucheza = mchezaji
- kusoma = msomaji
- kupenda = mapenzi
- kufundisha = mafunzo
- kucheka = kicheko

2.

- bora = kuboresha
- chafu = kuchafuka
- refu = kurefuka
- fupi = kufupisha
- nene = kunenepa

3.

- utendaji = mtendaji
- uongozi = kiongozi
- nyimbo = mwimbaji
- ufinyanzi = mfinyanzi
- maombi = mwombaji

FUNZO: UTUNGAJI WA RISALA (uk. 100)

Shabaha: Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya risala

Kuwaongoza wanafunzi kutunga risala

Kazi ya mwalimu	kazi ya mwanafunzi
Kueleza maana ya risala	kujigawa Katika makundi
Kuzungumza juu ya risala	kuwasilisha risala walizotunga
Kukumbusha mambo muhimu	Katika risala kuandika daftarini
Vifaa vitakavyotumiwa:	kitabu cha mwanafunzi
	Chaki
	Ubao

Majibu ya maswali

1 Vidokezi:

- Kuwasalimia viongozi kutokana na vyeo vyao kama sehemu mojawapo ya utangulizi.
- Kuorodhesha matatizo yanayowakumba wanafunzi wa darasa la sita kwa ujumla. Matatizo hayo wanafunzi watayataja katika aya kwa aya pamoja na mifano madhubuti inayoonyesha hasa hasa umuhimu wa mada yenyewe. Mambo haya yatajitokeza katika mwili.
- Baada ya kutaja matatizo, wanafunzi wataonyesha njia za kupata masuluhisho ya matatizo hayo kwa kutoa maoni yao kwa viongozi husika. Haya yatajadiliwa katika sehemu ya mwisho ambayo ni hitimisho.
- Kwa kumaliza wanafunzi watatoa shukrani zao kwa viongozi walioshiriki katika mkutano huo.

2. Vidokezi:

- Kutangulia na salamu kwa washiriki katika chama.
- Kuzungumzia historia ya chama cha kisasa nchini Rwanda na kuonyesha matatizo yaliyokikumba chama wakati huo.
- Kuwaelezea washiriki msimamo wa chama kutokana na maendeleo ya nchi.
- Kuwashukuru watu wote walioshiriki kama hitimisho la risala.

FUNZO: HOTUBA (uk. 101)

Shabaha: Kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya hotuba

Kuwaongoza wanafunzi kujua mambo yote kuhusu hotuba

Kazi ya mwalimu	kazi ya mwanafunzi
Kueleza maana ya hotuba	kufuata maelezo
Kuonyesha muundo wa hotuba	kufuata na kutoa maoni
Kueleza aina na sifa za hotuba	kusoma hotuba
Kuwafundisha mbinu za kutunga hotuba	kutunga hotuba

Vifaa vitakavyotumiwa:

Kitabu cha mwalimu

Chaki

Ubao

Majibu ya maswali

Swali la kwanza

Vidokezi:

- Kuonyesha heshima na taadhima kwa walimu na wazazi.
- Kutilia maanani maadili ya mafunzo ya kidini.
- Kuwa waaminifu, watulivu na wastahimilivu.
- Kutumia mavazi yenye staha na heshima.
- Kuwa na moyo wa ushirikiano.
- Kutoa msaada kwa wasiojiweza/ moyo wa ukarimu.
- Kuwa na moyo wa uzalendo.

Swali la pili

Vidokezi:

- Kuwanyima wanawake haki ya elimu.
- Kuwanyima wanawake haki ya kurithi ardhi na mali.
- Kutowashirikisha kikamilifu wanawake katika shughuli za maendeleo, uongozi na uamuzi.
- Kuoa wake wengi.
- Kubomoa majengo ya marehemu, kuharibu mali ya marehemu.
- Kuwafanyisha watoto kazi za sulubu.
- Kuwaoza nabinti au wasichana bila hari yao tena kabla hawajakomaa.

Swali la tatu

Vidokezi:

- Kutimiza kikamilifu mahitaji ya watoto: mavazi, malazi na chakula.
- Taifa kuwa na idadi ya watu linaloweza kuwapa huduma mathalani elimu na matibabu.
- Kupunguza tatizo la uhaba wa nafasi za ajira.
- Kupunguza janga la uharibifu wa mazingira kama vile ukataji wa miti kwa ajili ya makazi, makaa na nishati ya kuni.
- Kupunguza tatizo la watoto wazururao mitaani.
- Kuweza kujiendeleza, kujiwekea akiba.

Swali la nne

Vidokezi:

Mambo ya kufanywa ili kufanikiwa masomoni

- Kutia bidii masomoni.
- Kuwa na nidhamu na mwadilifu.

- Kutafuta ushauri na msaada kutoka kwa walimu na wazazi.
- Kujiwekea malengo ili yawe dira maishani.
- Kuwa mcha Mungu.

Umuhimu wa elimu

- Kuweza kuhitimu na kuendelea na masomo ya juu.
- Kupata ajira nzuri.
- Kumwezesha kuyaelewa mazingira na kuyadhibiti.
- Kuweza kuiongoza jamii.
- Kuweza kutangamana vizuri na watu wa jamii zingine.
- Kuweza kujiajiri na kujiendeleza kiuchumi.

MAREJEO

- Ndalu, A. (1997). Mwangaza wa Kiswahili, E. A. E. P Limited: Nairobi.
- Ngure, A. (2007/2006/2005/2004/2003). Fasihi simulizi kwa shule zasekondari, Phoenix Publishers: Nairobi.
- TUKI. (2004/2002/1993/1981). Fasihi Simulizi : Methali: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam.
- Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari. (1987). Kitabu cha Kiswahili IV-VC: Kitabu cha Mwanafunzi, Regie de l'Imprimerie Scolaire: Kigali.
- Kihore, Y. M. , Massamba, D. P. B. , Msanjila, Y. P. (2008/2007/2003). Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam.
- MASSAMBA, D. P. B, KIHORE, Y. M, Hokororo, J. I(2001/1999). SarufiMiundo ya Kiswahili Sanifu(SAMIKISA): Sekondari na Vyuo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam
- Bakhressa Salim, K. &Islam K. (1999/1998/1997/1996/1995). Kiswahili Sanifu: Darasa la saba, Oxford University Press: Oxford New York.
- Nelson. P, Scott. T& Judy P. (2007). Public speaking: a guide for the engaged communicator, M C Graw – Hill: New York
- Kearney, P. (1999). Public speaking in a diverse society: second Edition: MC Graw-Hill:New York
- Polycarp. S. W (2000). Uandishi wa Insha, Acacia Stantex Publishers.
- F. E. M. K. SENKORO (1988). Ushairi:Nadharia na tahakiki: Dar es Salaam University Press, Dar es salaam
- Mbunda, M. (1999). Uhakiki wa Fasihi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam

- Mbunda, M. (1993). Misingi ya uhakiki wa Fasihi, English Press Limited: Nairobi.
- TUKI. (2003). Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam
- Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari (1987). Kitabu cha Kiswahili IV B. Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari. Kigali.
- Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari (1987). Kitabu cha Kiswahili IV-VA. Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari. Kigali.